epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Desemba 13, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581889
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

UKURASA WA 3
**Bashungwa** aanza na mfumo ushughulikiaji malalamiko

UKURASA WA 4
**Kada** wa CCM atoa angalizo kukandamizwa kwa upinzani



UKURASA WA 18
**Janabi:** Muda ukifika nitasema, tuwasubiri WHO

UKURASA WA 18
**Kungwi** afariki dunia akienda kumfunda bibi harusi



UKURASA WA 22
GUARDIOLA HAELEWI KITU



# Lissu afunguka mazito kumvaa mwasisi Mbowe

• **Aanika** kisa na mkasa kukwepa mkutano wake kufanyikia makao makuu... *Endelea ukurasa 2*

## Mlima mwingine wameguka mkoani Manyara, ekari 10, nyumba zaathirika


UKURASA 3



Ezekia Wenje



Godbless Lema



John Heche



Wananchi wa kijiji cha Moya Mayoka, kata ya Magara, wilayani Babati, mkoani Manyara, wakiwa kwenye taharuki baada ya kutokea maporomoko ya tope na mawe kutoka mlima Magara jana. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Tume ya Kodi yakutana na vigogo kumulika yaliyojificha

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA YAIFUATA MAZEMBE, MATUMAINI TELE** UK.24 **KATUNI** UK.6



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akisalimiana na wanachama wa chama hicho, baada ya kuzungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana. **PICHA: RESTUTA JAMES**

# Lissu afunguka mazito kumvaa Mbowe

**Na Restuta James**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amepandisha joto ndani ya chama hicho baada ya kutangaza kugombea uenyekiti wa wa taifa huku akisimamia ajenda saba.

Kwa kutangaza huko, Lissu atamvaa Mwenyekiti wa CHADEMA aliyeko madarakani, Freeman Mbowe. Lissu alitangaza azma hiyo kwenye mkutano wake na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, ambao pia ulihudhuriwa na wawakilishi wa kanda nane za CHADEMA, akiwa na kaulimbiu ya 'Nuru Mpya, Mwelekeo Mpya, Mapambano Mpya.'

Lissu alisema ikiwa atashindwa kwa haki kwenye uchaguzi huo, atabaki kuwa mwanamageuzi na atakubali matokeo na kusisitiza kwamba hayuko tayari kuharibu chama alichokijenga kwa jasho na damu kwa miaka 20.

"Nikishindwa kwenye uchaguzi huru na haki sitakuwa na cha kusema. Kukiwa na mambo ya kihuni, kuna mtu ataniambia nisilie, ninyamaze, sitanyamaza," alisema huku akisisitiza hana mgogoro na Mbowe japokuwa wamekuwa wakitofautiana kwenye baadhi ya mambo.

Alitoa mfano kwamba hakukubaliana naye kwenye suala la maridhiano na CCM na kwamba anaamini ulikuwa msimamo sahihi.

**AGENDA ZAKE SABA**

Alisema agenda yake ya kwanza ni kufanya siasa katika kile alichoita mazingira mapya, ambayo yalianza baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Alisema tangu mwaka 2015, Tanzania iliingia kwenye utawala usiokubali ushindani kupitia uchaguzi huru na haki.

Lissu ambaye ni mwanasheria kitaaluma, alisema nchi iko kwenye kipindi cha siasa za kidhalimu, zinazotumia vyombo vya dola kukisaidia Chama Cha Mapinduzi (CCM), kushinda uchaguzi.

Aina hiyo ya siasa, alisema imefanikisha CCM kuongoza mitaa, vijiji na vitongoji vyote mwaka 2019, wabunge na madiwani wengi kutokana na CCM kwenye uchaguzi mkuu mwaka 2020 na kushinda kwa kishindo uchaguzi wa mwezi uliopita.

Kwenye uchaguzi uliofanyika mwezi uliopita, alisema wagombea wengi wa upinzani walienguliwa kwa madai ya kukosa sifa kama ilivyofanyika mwaka 2019.

Lissu alisema ili kushindana kwenye hali ya sasa, CHADEMA inahitaji kuendelea kudai Katiba Mpya ya Kidemokrasia, Mfumo Mpya wa Uchaguzi wenye Tume Huru, Sheria Bora ya Uchaguzi na haki kwa watu wote.

Kwa mujibu wa Lissu, agenda yake ya pili ni kuisuka upya katiba ya CHADEMA ili kuweka ukomo wa madaraka ya uongozi ndani ya chama hicho na kwa wabunge na madiwani wa viti maalum.

"Pia kuweka ukomo wa madaraka katika uongozi wa chama si tu utaondoa uwezekano wa viongozi kung'ang'ania madaraka, bali utawezesha kujengeka kwa utamaduni wa kuandaa viongozi wapya wa chama wa kila kizazi.

"Ukomo wa madaraka utapunguza sana, kama si kuondoa kabisa, upambe na uchawa unaoshamiri pale viongozi wanapong'ang'ania madaraka katika mazingira yasiyokuwa na ukomo wa Madaraka," alisema.

Kuhusu ukomo katika nafasi za viti maalum, alisema zitawawezesha wanawake kupata uzoefu na uwezo wa kisiasa na kiuchumi katika shughuli za bunge na halmashauri za serikali za mitaa.

Lissu alitaja agenda nyingine kuwa ni kuweka mfumo wa uchaguzi ndani ya chama, ambao utaundwa ndani ya Katiba ya chama hicho.

Alisema lengo ni kupata viongozi waadilifu na wanaoweza kuendesha siasa katika mazingira ya sasa na kuweka mkazo wa kuheshimu taratibu za uchaguzi katika ngazi zote, ili kuondoa mipasuko.

"Kuacha kuzingatia na kuheshimu Katiba ya chama ni kukaribisha kila aina ya uhuni, rushwa, uonevu na mambo ya hovyo katika uendeshaji wa chaguzi za chama chetu.

"Kama ambavyo tunahitaji Tume Huru ya Uchaguzi na mfumo huru wa uchaguzi katika chaguzi zetu za umma, ndivyo tunavyohitaji chombo huru cha kusimamia chaguzi zetu za ndani ya chama," alisema.

Alisema lengo ni kuwahakikishia wagombea wa nafasi mbalimbali kuwa watatendewa haki na wasimamizi wa uchaguzi katika hatua zote za mchakato wa uchaguzi.

"Haya yote yanawezekana endapo tutarekebisha Katiba yetu ya chama ili kuweka mfumo huru wa kusimamia chaguzi za chama," alisema.

Agenda nyingine ni kuweka utaratibu mpya wa kutafuta, kusimamia na kutumia fedha na rasilimali za chama hicho. Alisema utaratibu wa sasa umeweka utegemezi kwa watu wachache ndani ya chama kutafuta fedha na rasilimali za chama.

**KWA NINI LISSU?**

Alisema amejipima na kuona anafaa kuongoza chama hicho ngazi ya taifa kwa kuwa ana historia ya uadilifu na kukubalika na jamii.

"Napenda kuamini kwamba historia ya uadilifu wangu na kukubali kwangu na jamii ya Watanzania inajulikana wazi na Watanzania walio wengi. Hatua hii ya mapambano inahitaji kiongozi aliyeonyesha kwa tabia, mwenendo wa uzalendo wa kupenda na kutetea nchi yake na msimamo wa kuaminika.

"Uzalendo wangu na msimamo wangu umepimwa na kuthibitishwa katika mapito na majaribu mengi ambayo nimepitishwa takribani miongo mitatu ya maisha yangu ya utetezi wa haki za wananchi wetu, na rasilimali za nchi yetu. Kwa sababu hizo, ninaamini nina sifa hizo mahsusi na nyingine zilizotajwa katika Katiba yetu ya chama.

"Uzoefu wangu wa kitaaluma na kisiasa; kwa historia yangu ya utumishi katika chama, bungeni na kwingineko, na kwa msimamo wangu thabiti na usiotetereka, ninazo sifa na uwezo wa kusimamia maboresho yote yanayohitajika katika uendeshaji bora wa shughuli za chama chetu katika kipindi hiki kigumu," alisema.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Wananchi walalamikia kero kiwanda kutiririsha majitaka

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

WAKAZI wa Mtaa wa Vitendo Kata ya Misugusugu, Halmashauri ya Mji wa Kibaha mkoani Pwani wamelalamikia kiwanda kinachozalisha kemikali za kutengenezea pombe kali kutiririsha maji machafu yenye harufu kali yanayopita katika makazi ya watu na mashamba.

Maji hayo yanadaiwa kuleta madhara kwenye mashamba ambayo yalikuwa yanalimwa mpunga na kusimamisha shughuli za kilimo, huku harufu kali ikiwa kero nyakati zote kwa wanaoishi karibu na kiwanda hicho.

Kuwapo kero hiyo kulianza kuelezwa na Mchungaji Sixtus Malya katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha kilichofanyika hivi karibuni kikiongozwa na Mwenyekiti ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson John.

Malya alieleza namna wananchi wanavyoteseka na maji hayo huku waliokuwa wakifanya shughuli za kilimo kusimama kutokana na uwingi wa maji hayo meusi yanayoua mimea.

Nipashe ilifunga safari mpaka eneo hilo ikianzia kwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Vitendo na baadaye kufika kwenye maeneo yanayotiririsha maji hayo kutoka kiwandani ambapo kuna mabomba yaliyoelekezewa shambani.

Maji machafu yanayotiririka kutoka kiwandani yamewekewa mabomba ambayo yanaelekea kwenye mashamba ya wananchi na bonde walimokuwa wakitumia wakazi wa eneo hilo kwa kilimo cha mpunga ambalo lipo jirani na makazi ya watu.

Wakizungumzia kuhusiana na kero hiyo baadhi ya wakazi wa eneo hilo la kiwanda akiwemo Ditrick Haule, Juma Meena, Winning John na Mwamvuta Shubet walisema malalamiko yao wamekuwa wakiyafikisha kwa viongozi lakini bado hayajapatiwa ufumbuzi.

Haule alisema maji hayo machafu yameathiri maeneo yao ya kilimo na kwamba mbali ya mabomba yaliyoelekezewa bondeni pia wakati mwingine kuna magari ya kiwanda hicho yamekuwa yakibeba maji machafu kutoka kiwandani na kuyamwaga barabarani.

Naye, Juma Meena alieleza kwamba endapo angekuwa na uwezo wa kuuza eneo lake angefanya hivyo ili kuondokana na kero ya harufu kali wanayokumbana nayo. Winni John alisema katika eneo hilo wanakosa hewa safi kutokana na harufu kali zinazotoka kwenye maji yanayotiririka sambamba na kelele ambazo zinawaathiri wanafunzi Shule ya Sekondari Misugusugu iliyokaribu na kiwanda hicho.

Bahati Mbaigwa ameomba serikali kuingilia kati ikiwezekana kuhamisha shule hiyo kwani wanafunzi wanaosoma katika shule hiyo wakati mwingine wanashindwa kuhimili harufu kali wakiwa darasani.

Mmoja wa wananchi wa Mtaa wa Vitendo ambaye hakutaka kutajwa jina lake alisema wapo wananchi wanaumwa koo na wanafunzi wengine wanaomba kuhama kutokana na kushindwa kuhilimi kero zinazotokana na kiwanda hicho.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Vitendo, Ally Lunga alithibitisha kuwapo malalamiko hayo kutoka kwa wananchi huku akiomba kiwanda hicho kufanya marekebisho ya kuondoa harufu na kuweka mfumo wa utirishaji maji yanayotoka kiwandani.

Akiwa katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson John alikiri kufahamu kero ya kiwanda hicho huku akiahidi kuwa wilaya inalisughulikia ili kumaliza tatizo hilo.

Mwandishi aliutafuta uongozi wa kiwanda, lakini haukuwa tayari kuzungumzia hatua wanazochukua kukabiliana na hali hiyo.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Buriani (wa pili kulia), akiangalia bidhaa mbalimbali zinazotengenezwa na wajasiriamali vijana, kabla ya kufungua Kongamano la Vijana 2024, lililoandaliwa na Taasisi ya GOYN kwa kushirikiana na Mradi wa Tanga Yetu na Five Brothers Entertainment, jijini Tanga jana, lenye lengo la kuwainua vijana wa mkoa huo, lenye kaulimbiu ya "Vijana ni Fursa: uwezeshwaji na kukuza fursa za vijana". **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tume ya Kodi yakutana na vigogo kumulika yaliyojificha

**Na Gwamaka Alipipi**

WADAU na wafanyabiashara kutoka sekta mbalimbali wamewasilisha maoni, kero na changamoto zinazowasibu kwenye Tume ya Rais ya Marekebisho ya Kodi, ikiwamo makato makubwa ya kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Oktoba 4, mwaka huu, Rais Samia aliunda tume hiyo lengo likiwa ni kuboresha ukusanyaji wa kodi na kuhakikisha ufanisi katika matumizi yake pamoja na kushughulikia changamoto zinazoathiri mfumo wa kodi nchini.

Lengo lingine ni kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa kodi, jambo ambalo litajenga imani zaidi kati ya wananchi na serikali.

Wakizungumza katika mkutano huo, baadhi ya wafanyabiashara waliwatupia lawama maofisa wa TRA kutokuwa na maadili ya kazi wanapokwenda kukusanya kodi hizo.

**TUCTA**

Mjumbe kutoka Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Pasco Lugaga, alisema kuna upendeleo katika makato ya kodi kwenye posho za watumishi.

Alisema kuna baadhi ya watumishi ambao wanakatwa na wengine hawakatwi na aliomba kuwapo na usawa kwa watu wote.

**CWT**

Mwekahazina wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya ya Temeke, Hassan Haruna, aliiomba serikali kushusha makato ya kodi ya mshahara hadi dijiti moja.

"Maadili ya ukusanyaji wa kodi kwa maofisa wa TRA ni changamoto sana. Utakuta watumishi wanaokwenda kukusanya kodi wengi wao hawana maadili," alisema Haruna.

**SHIVYAWATA**

Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Charles Temba, alisema mfumo wa kodi wa TRA haujakaa vizuri na kuomba kuwekwe mfumo ambao hautasumbua.

"Ukikamatwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) unaambiwa lipa Sh. 100,000 na ukikamatwa na TRA unaambiwa acha bajaji mpaka utakapomaliza kodi, wanaomba ulipe nusu ya kodi," alisema.

**JUMUIYA WAFANYABIASHARA**

Katibu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Renatus Mlelwa, alisema makato ya kodi ya mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam ni makubwa kulinganisha na nchi jirani.

"Ukitoa kontena la thamani ya Sh. mil 400 kodi yake ni Sh. milioni 200. Ukienda Bandari ya Mombasa Kenya gharama ni Sh. milioni 50. Mwaka jana kontena la vitenge ilikuwa Sh. milioni 350 na ndio maana wanalalamika sheria haziandikiki ni kwa sababu hiyo mfumo wa forodha ni changamoto," alisema.

"Ukienda TRA mfumo wa VAT wafanyabiashara ndio wanawadai TRA, hivyo nashauri tuweke sheria zinazoendana na wafanyabiashara wetu tusiige sheria za nje sisi bado tunakua."

Kadhalika, aliishauri tume hiyo kuwaangalia kwa jicho la tatu wafanyabiashara wanaoingiza mashine za EFD kwa sababu wao ndio vinara wa kuzichezea mashine hizo.

Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Mfaume Fadhili alisema: "Sheria inampa mamlaka ofisa wa TRA kukadiria kutokana na kile anachokiona, hivyo hata iweje hii vita haiwezi kuisha ya maadili ya rushwa kwenye kukusanya kodi kwa sababu vifungu vingi vina utata, hivyo tunaomba vifanyiwe marekebisho."

Mwakilishi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Taifa, Fredick Lutindi alisema eneo la Bandari ya Dar es Salaam kuna tatizo kubwa la mfumo wa forodha.

Aliomba kuwapo na kiwango kimoja cha tozo ya kodi, kusiwe na utofauti wa viwango katika mizigo inayoshuka katika bandari hiyo.

Alisema eneo la Kariakoo kumekuwa na wamachinga wengi, na kwamba serikali inapaswa kuwatengenezea maeneo yao maalumu, kwamba wakusanya kodi wamekuwa wengi kuliko wateja.

Awali, akifungua kikao hicho, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Balozi Ombeni Sefue, alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliunda tume hiyo lengo likuwa ni kufanya tathmini na kuleta mapendekezo ya nini cha kufanya.

Alisema tume hiyo iliundwa baada ya malalamiko kadhaa ya wafanyabiashara ikiwamo kubambikiziwa kodi. Alisema tume hiyo itafanya kazi Tanzania Bara na Zanzibar ili kusaidia ongezeko la mapato kwa serikali kwa njia rafiki.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Bashungwa aanza na mfumo ushughulikiaji malalamiko

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Innocent Bashungwa, ameagiza menejimenti ya wizara hiyo kusimamia kitengo kinachoshughulikia malalamiko yanayotolewa kwa wizara, taasisi na vyombo vya usalama, kuhakikisha kinayafanyia kazi na kutoa mrejesho wa utatuzi wa malalamiko kwa wananchi.

Bashungwa pia amevitaka vitengo vya mawasiliano na habari vya wizara, vyombo vya usalama na taasisi zote kuboresha mfumo wa mawasiliano na habari kwa umma.

Alielekeza hayo jana wakati akizungumza na wakuu wa idara na vitengo mara tu baada ya kupokewa Makao Makuu ya wizara yaliyoko Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma na kusisitiza kuwa ni haki ya watanzania kupata taarifa sahihi kwa wakati.

"Kuna malalamiko mengine yanakuwapo kwa sababu hamna taarifa sahihi au taarifa imechelewa. Kwa hiyo, lazima mhakikishe mnashughulikia malalamiko na kutoa mrejesho," aliagiza Bashungwa.

Vilevile, Bashungwa aliwaomba watumishi wa wizara hiyo kutoa ushirikiano kwake na viongozi wengine wote ili kwa pamoja watimize adhima ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwahudumia wananchi.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo alimkaribisha Waziri Bashungwa na kumhakikishia ushirikiano wa karibu katika utekelezaji majukumu katika wizara hiyo.

Nipashe
WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu

# Mlima waporomoka nyumba zazingirwa tope, mawe

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

ZAIDI ya nyumba 15 zenye wakazi zaidi ya 30 katika Kijiji cha Moya Mayoka, kata ya Magara, wilayani Babati, mkoani Manyara, zimezingirwa na mawe na tope lililoshuka kutoka Mlima Magara na kusababisha wananchi kukimbia tope.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, Diwani wa Kata ya Magara, Jacob Bilikuli alisema tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 1:00 asubuhi.

"Eneo ambalo mawe na tope vimeshuka mpaka kwenye makazi ya wananchi ni zaidi ya ekari 10 ambapo mawe na tope vimeharibu nyumba za wananchi," alisema Bilikuli.

Aidha, alisema athari zingine zilizopatikana ni mifugo na vyakula kusombwa na maji na kufunikwa tope na mawe.

Alisema baada ya kutokea maafa hayo waliwahamisha wananchi waliopoteza makazi na kuwahifadhi Shule ya Msingi Moya Mayoka.

Pia, alisema wanaendelea kumsubiri Mkuu wa Wilaya ya Babati, Emmanuela Kaganda ili washauriane cha kufanya.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Magara, Hawa Nyoni akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Manyara, Lucas Mwakatundu, alipoulizwa kwa njia ya simu kuhusu tukio hilo, alisema hajapata taarifa na kuahidi kufuatilia ili kujua ukweli wa tukio hilo.

Kijiji cha Moya Mayoka kinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Mdau wa Maendeleo Jimbo la Vunjo, mkoani Kilimanjaro, Enock Koola (kulia), akipongezwa na Msaidizi wa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini, Mchungaji Deogratius Msanya, baada ya kuchangia Sh. milioni 6 za ujenzi wa maktaba ya Shule ya Seminari ya Agape, kata ya Mamba Kusini, wilaya ya Moshi, juzi. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Mbunge mstaafu atoa angalizo kuhusu upinzani kukandamizwa

**Na Mussa Mwangoka,**
MPANDA

KADA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mbunge mstaafu wa Mpanda Mjini, Said Amour Alfi, amesema ni makosa makubwa kushabikia kukandamizwa kwa vyama vya upinzani katika uchaguzi mbalimbali nchini.

Amesema kuwapo kwa wawakilishi wake katika nyadhifa mbalimbali ni chachu ya kuchagiza maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Kada huyo ambaye aliwahi kuwa Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Tanzania Bara na mbunge wa Mpanda kwa miaka 10 kupitia chama hicho kabla ya kuhamia Chama Cha Mapinduzi (CCM) alisema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa Habari nyumbani kwake, mjini hapa.

"Sisi Chama Cha Mapinduzi tutafanya makosa makubwa sana kama tutatumia rasilimali zetu na nguvu zetu na maarifa yetu kuua upinzani. Lazima tuache upinzani ukue kwa kuwa una faida nyingi sana katika ustawi wa taifa hili," alisema.

Alitolea mfano wakati wa utawala wa awamu ya nne, ambapo mikoa ya kanda magharibi kwa maana ya Rukwa, Katavi, Tabora na Kigoma ilikuwa haijafunguka kimiundombinu, hivyo kutofikika kiurahisi, lakini nguvu ya vyama vya upinzani ilisaidia Serikali kuifungua mikoa hiyo.

Alisisitiza kua upinzani ni kichocheo cha maendeleo na ni fursa kwa upande wa pili kuieleza na kuikosoa serikali kuhusu kasoro zilizopo na hatua stahiki zinazopaswa kuchukuliwa.

Kwa mujibu wa Arfi, awamu ya tano ndiyo iliyojielekeza kuumaliza upinzani na ilifaulu kufanya hivyo, hali ambayo ilisababisha kutokuwapo watu au wanasiasa wanaokosoa serikali, kitu ambacho ni hatari kwa ustawi wa maendeleo ya taifa.

"Niwaeleze wana CCM wenzangu, tutakuwa tunajidanganya kama tutaamini kwamba tumeua upinzani. Kiuhalisia upinzani hauonekani ila upo katika mioyo ya watu, hivyo tusijidanyanye," alisema.

Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, alisema kwa maoni yake hakufurahishwa na mchakato mzima ikiwa ni pamoja na matokeo yake.

Alisema watendaji wa walifanya mambo ambayo hawakuagizwa na CCM, bali kwa matakwa yao binafsi tu wakawakandamiza wapinzani.

"CCM isiwe sababu ya kukandamiza demokrasia. Tutoe haki kwa hivi vyama na isivyo bahati sana, CCM wakati mwingine inahusishwa katika haya mambo ni kutokuwa na uaminifu na dhamira njema ya kutazama hii nchi kama ni nchi yetu sote.

"Viongozi wanaosimamia uchaguzi ndio chanzo cha mifarakano yote, na wao ndio wanaruhusu kura feki kuingia katika masanduku, wasiokuwa na haki wanapiga kura. Tuwaeleze watendaji wetu watende haki. Bila kuwapo haki tutaliua hili taifa na si vinginevyo," alisema.

Arfi alishauri kuwa kasoro zilizojitokeza katika uchaguzi huo zisijirudie ili Uchaguzi Mkuu ujao uwe huru na haki na kuondoa malalamiko yasiyo na tija kwa wananchi na vyama vya siasa vya upinzani.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alitangaza matokeo ya jumla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba 27 mwaka huu, akisema kuwa CCM ilipata ushindi wa jumla wa wenyeviti wa serikali za vijiji kwa nafasi ya viti 12,150 sawa na asilimia 99.01.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*


CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: ...............OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

OLYMPIC PETROLEUM (T) LTD. 30823... ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Petrol Station Manager, Olympic Petroleum (T) Limited, Plot No. P28250, Segerea Area, Ilala Municipality, DSM City

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the ...19... day of ...December... 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this ...28... day of ...Novemba... 2024

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

218295802


## WB yaimwagia Tanzania bil. 257/-

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya Dunia (WB) imeipatia Tanzania msaada wa Dola za Marekani milioni 104 (Sh. bilioni 257.14) kusaidia utekelezaji wa mradi wa kukuza usawa wa kijinsia kwa wanawake uitwao 'Pamoja'.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana baada ya utiaji saini wa makubaliano hayo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema mradi huo unatarajia kuwanufaisha wanawake 319,850 Tanzania Bara na Visiwani

Alisema mkataba huo ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa 2021/22 - 2025/26. Pia ni sehemu ya Rasimu ya Dira ya Maendeleo ya 2050 na ajenda kuu ya serikali ya kuipa suala la usawa wa kijinsia kipaumbele.

Dk. Nchemba alisema mradi huo utasaidia kuongeza upatikanaji wa fursa za kiuchumi kwa wanawake pamoja na huduma za kuzuia na kukabiliana na ukatili wa kijinsia Tanzania Bara na Zanzibar.

"Hili litatimizwa kupitia uimarishaji vikundi vya wanawake kwa kuwajengea ujuzi wa biashara na kuwaunganisha na fursa za masoko; kuongeza fursa za mikopo nafuu kwa vikundi vya wanawake; kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wanawake kupitia mifumo rasmi ya kifedha," alisema. Alitaja lengo lingine ni kuimarisha huduma za kukabiliana na ukatili wa kijinsia, kwamba wanawake 319,850 watanufaika moja kwa moja na walengwa wengine 399,000 wakiwemo wajumbe wa kaya za wanufaika.

Pia alisema suala la kukuza usawa wa kijinsia siyo la wanawake peke yao bali ni msingi wa taifa la kidemokrasia lenye haki na linalostawi, kwamba kuondoa tofauti za kijinsia kunaboresha uzalishaji na kuimarisha uhimilivu wa kiuchumi.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema mradi huo utawawezesha wanawake kiuchumi na kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Dk, Gwajima alisema mradi wa pamoja una maeneo makuu manne ambavyo ni kukuza fursa za kiuchumi kwa wanawake, kuimarisha huduma za kuzuia na kukabiliana na ukatili wa kijinsia, ubunifu na ushirikiano pamoja na usimamizi, ufuatiliaji na tathmini. Alisema manufaa ya utekelezaji huo ni pamoja na kusaidia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023 katika kutokomeza vitendo vya ukatili na kuwawezesha wanawake kiuchumi.

Manufaa mengine, alisema ni kuwezesha utekelezaji maono mapana ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuhusu Jukwaa la Kizazi chenye Usawa (GEF) ambapo yeye (Rais) ni kinara wa eneo namba mbili la haki na usawa wa kiuchumi ambalo linalenga kuwawezesha wanawake kiuchumi.

Alisema pia kuwezesha utekelezaji wa mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kuwezesha ujenzi wa nyumba salama 10

Dk. Gwajima alisema pia utawezesha ujenzi wa vituo 200 vya malezi ya watoto wadogo Tanzania bara 184 na Zanzibar 16, ujenzi na ukarabati wa ofisi 40 za maafisa ustawi wa jamii (vituo vya ushauri) na ofisi 40 za maofisa maendeleo ya jamii.

Vilevile, alisema utawezesha kununua vifaa vya ofisi na vitendea kazi kwa maofisa maendeleo ya jamii na maofisa ustawi wa jamii.

## HABARI KITAIFA

# Kisena, wenzake wakana mashtaka yanayowakabili

**Na Kulwa Mzee**

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Usafirishaji wa Mabasi Yaendayo Haraka (UDART), Robert Kisena, na wenzake wawili wamekana kutumia Sh. bilioni 4.4 kulipa madeni ya kampuni yao ya Simon Logistics Group Ltd na Simon Group Ltd, hivyo kusababisha UDART kupata hasara ya kiasi hicho cha fedha.

Kisena na wenzake walikana mashtaka hayo jana katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Sedikia Kisanya, wakati upande wa Jamhuri ukiwasomea maelezo ya awali.

Wakili wa Serikali, Dickson Shayo, aliwataja washtakiwa wengine kuwa ni Charles Newe aliyekuwa Mkurugenzi wa Shirika la Usafiri Dar Es Salaam (UDA) na UDART, Kulwa Kisena Mtendaji Mkuu wa Simon Group na Simon Logistics Group, Simon Group na Simon Logistics.

Wakili Shayo alidai kuwa Kisena ni mfanyabiashara, alikuwa Mkurugenzi wa UDA na UDART, mkurugenzi na mwanahisa wa Simon Group na Simon Logistics na anaishi Upanga, Mtaa wa Isevya, Ilala, Dar es Salaam.

Alidai mshtakiwa Newe ni mfanyabiashara, alikuwa Mkurugenzi wa UDA, UDART, Mtendaji Mkuu Simon Group na mkazi wa kijiji cha Isole Buyagu wilayani Sengerema, Mwanza.

Mshtakiwa wa tatu, Kulwa alidaiwa alikuwa Mkurugenzi wa Simon Logistics na Simon Group na mkazi wa Dar es Salaam.

Ilidaiwa kuwa Kampuni ya Simon Logistics na Simon Group ni kampuni za wanahisa zilizosajiliwa Tanzania mwaka 2007 na 2013.

Washtakiwa wote baada ya kusomewa majina yao na nyadhifa walizokuwa nazo, walikubali ni kweli lakini walikana maelezo mengine yote kuhusiana na mashtaka yanayowakabili ya kuongoza genge la uhalifu, kughushi, kuwasilisha nyaraka za uongo, kutakatisha fedha na kusababisha hasara ya Sh. 4,460,082,311 kwa UDART.

Wakili Shayo alidai Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ilianza uchunguzi baada ya kupata taarifa kwamba Kisena na Newe wanatumia mapato ya UDART kwa ajili ya kulipa madeni ya Simon Group na Simon Logistics .

Alidai uchunguzi ulibaini mwaka 1983 UDA ilikuwa inamilikiwa na serikali ikiwa na mtaji wa hisa milioni 15, hisa 7,119,697 ziligawiwa na hisa 7,880,303 hazikugawiwa.

Wakili Shayo alidai serikali kupitia Hazina ilihamishia hisa 3,631,046 sawa na asilimia 51 kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na hisa 3,488,651 sawa na asilimia 49 zilibakia Hazina.

Alidai Machi 11, 2011 Kisena na Simon Group kwa udanganyifu walijipatia hisa zote ambazo hazikugawiwa zenye thamani ya Sh 1,142,643,935 sawa na asilimia 52 za UDA na kusababisha Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kubakiwa na asilimia 24.

"Baada ya Simon Group kuwa mwanahisa mkuu kwa kuchukua hisa zote za UDA, mshtakiwa Kisena na Newe walikuwa wakurugenzi na watia saini wa kampuni ya UDA.

"Septemba 25, 2013 Simon Group ilinunua hisa zote za halmashauri 3,631,046 na Septemba 19 2014 mshtakiwa Kisena alisajili kampuni mpya UDART ambapo UDA ilikuwa inamiliki hisa 14,850 sawa na asilimia 99 na Simon Group ilikuwa inamiliki hisa 150 sawa na asilimia moja.

"Mei 24, 2015 UDART aliingia mkataba na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kuwa wakala wa kuendesha mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi na Juni 11, 2015 mshtakiwa wa kwanza, pili na wa tatu walighushi miniti za kikao cha Bodi ya Wakurugenzi kuonyesha mshtakiwa Kisena na Newe ni watia saini katika akaunti mbili zinazomilikiwa na UDART Benki ya NMB Tawi la Benki House," alidai.

> **"Baada ya Simon Group kuwa mwanahisa mkuu kwa kuchukua hisa zote za UDA, mshtakiwa Kisena na Newe walikuwa wakurugenzi na watia saini wa kampuni ya UDA.**

Alidai kua washtakiwa waliwasilisha nyaraka za kughushi benki na kati ya Septemba 19, 2017 na Januari 30, 2019 Kisena, Newe na Kulwa walitumia fedha za UDART kulipa madeni ya Simon Group na Simon Logistics na kusababisha kampuni hiyo kupata hasara zaidi ya Sh. bilioni nne. Machi 17 na Agosti 15, 2017 Newe ilidaiwa kuwa alimwandikia barua Mtendaji Mkuu wa NMB akimwomba waunganishe madeni yote ya Simon Group na Simon Logistics katika akaunti moja yalipwe na Simon Logistics huku Simon Group ikibakia kuwa mdhamini.

Alidai Septemba 15, 2017 na Januari 31, 2019 Kisena na Newe wakiwa watia saini katika akaunti za UDART, walielekeza NMB kuhamisha fedha katika akaunti hiyo kwenda akaunti ya Simon Logistics inayomilikiwa na Simon Group kama marejesho ya mkopo wakati hakukuwa na makubaliano na mshtakiwa wa nne kulipa madeni ya Simon Group kwa kutumia fedha za UDART.

Wakili Shayo alidai mshtakiwa 1 na 2 walihamisha miamala yote katika akaunti ya UDART kwenda kwenye akaunti ya Simon Logistics ltd na Simon Group huku wakijua kufanya hivyo ni mazalia ya kosa la kughushi.

Machi 7 mwaka 2019 alidai John Xavery aliyekuwa Mkurugenzi UDART alimwandikia barua Mkurugenzi Mtenda NMB akimwelekeza kuacha kutumia fedha za UDART kulipa madeni ya Simon Group na Simon Logistics.

Alidai kwa vitendo hivyo washtakiwa wote walisababisha UDART kupata hasara ya Sh. 4,460,082,311. Baada ya kumaliza kusoma maelezo hayo Jaji Kisanya alisema hakuna ubishi kwamba washtakiwa walikubali majina na nyadhifa zao na kukana maelezo mengine yote dhidi ya mashtaka yanayomkabili.

Upande wa Mashtaka ulidai katika kuthibitisha mashtaka dhidi ya washtakiwa watakuwa na mashahidi 26 na vielelezo 85 na.upande wa utetezi walikubaliwa kuongezewa muda wa kuwasilisha orodha ya mashahidi.

Mahakama iliwaamuru kuwasilisha orodha ya mashahidi kabla ya Desemba 27, mwaka huu, na shauri lotaanza kusikilizwa baada ya kupangiwa tarehe. Washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu gerezani.

**The Guardian Limited**

**VACANCY**

**Sales Freelancers**

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales Freelancer to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, ( Moshi, Arusha, Tanga, Morogoro, Iringa, Mwanza and Zanzibar)**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

182777

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15st December, 2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA ARUSHA, KILIMANJARO NA DODOMA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA CHEMBA, KONDOA NA MJI WA KONDOA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dodoma katika Halmashauri za Wilaya za Chemba, Kondoa, na Mji wa Kondoa kuanzia tarehe 11 hadi 17 Desemba, 2024. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. SIKU: Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 11 hadi Jumanne tarehe 17 Desemba, 2024.
2. VITUO: Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. MUDA: Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 8 na kubonyeza, baada ya hapo atachagua namba 2 na kubonyeza, Kisha atachagua namba 3 (Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi) na hapo, atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 03 Desemba, 2024 na:

**Livini A. Morrice**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

218284201

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni wakati mwafaka kwa wanaume kupaza sauti dhidi ya manyanyaso

**VITENDO** vya ukatili wa kijinsia vimekuwa vikishamiri mwaka hadi mwaka ndani ya jamii na hata kuacha maumivu yasiyoisha kwa baadhi ya watu. Miongoni mwa vitendo hivyo ni ukatili wanaofanyiwa wasichana na wavulana wa kazi dhidi ya mabosi wao, vipigo kwa wanawake kutoka kwa wenzi wao na hata vifo, ukeketaji na mauaji ya vikongwe.

Kutokana na kushamiri kwa vitendo hivyo, wadau wa haki za binadamu wamekuwa wakijitokeza hadharani na kulaani hata kuweka mikakati ya kuzuia kuendelea kutokea. Moja ya mambo yaliyofanikiwa na wanaharakati hao ni kutungwa kwa sheria ya makosa ya kujamiiana, ambayo wanaokutwa na hatia adhabu yao ni kifungo cha miaka 30 jela.

Kwa muda mrefu, sehemu kubwa ya jamii imekuwa ikidhani kuwa wanaofanyiwa vitendo hivyo vya kikatili ni wanawake na watoto na lawama nyingi kuelekezwa kwa kinababa.

Ukweli ni kwamba wako baadhi ya wanaume wanaofanyiwa vitendo hivyo na wenza wao na wakati mwingine kwa kushirikiana na watoto. Moja ya mifano ya matukio hayo ni wanawake kuwakimbia waume zao huku wakiondoka na mali zote na kuwaacha watupu.

Wanaume hao wamekuwa wakinyimwa unyumba, kupigwa na kunyanyaswa na wenza wao huku wakishindwa kupaza sauti dhidi ya vitendo hivyo. Sababu kubwa inayowafanya kukaa kimya au kutoripoti matukio hayo ni kudhani kwamba wanaweza kudharauliwa na jamii.

Hali hiyo imewafanya wengi kukaa na machungu moyoni huku wakipata maradhi yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari, shinikizo la damu, msongo wa mawazo na tatizo la afya ya akili.

Unyanyasaji huo dhidi ya wanaume umekuwa ukitokana na baadhi yao kuporomoka kiuchumi au mwanamke kuwa na uwezo wa kiuchumi dhidi ya mwanamume.

Matokeo yake wanaume wamekuwa wakidharauliwa na hata kupewa majina kama 'mwanamume suruali' au 'kula kulala'.

Siku hizi, ni jambo la kawaida kumkuta mwanamume barabarani akizungumza peke yake huku hali yake ikiwa dhaifu. Miongoni mwa sababu zinazochangia hali hiyo ni kuporomoka kiuchumi, kukosa kazi au kuachishwa kazi ambayo ilikuwa ikimpatia riziki yake na familia kwa ujumla. Hapo pia manyanyaso dhidi yake ndani ya nyumba kutoka kwa mwenza na familia yanaibuka.


Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) kimewataka wanaume kuacha kulia majumbani wanapofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na wake zao, badala yake watoe taarifa kwenye vyombo vya kisheria yakiwamo madawati ya jinsia.

Chama hicho wakati wa mdahalo wa Siku ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia juzi jijini Dodoma, kilibainisha kwamba bado kuna wanaume wanafanyiwa vitendo vya kikatili lakini wanaishia kulia ndani ya nyumba, hivyo kutakiwa watoe taarifa ili wapatiwe msaada wa kisheria.

Wahenga wanasema ukimya wako umaskini wako na kimya chako ni mauti yako. Kwa mantiki hiyo, wanaume wanaonyanyaswa kuendelea kunyamazia vitendo hivyo kuna madhara makubwa dhidi yao. Ndiyo maana kumekuwa na matukio ya baadhi ya wanaume kuchukua uamuzi mgumu kama kuwaua wenza wao na kisha kujiua kutokana na kukaa na mambo moyoni bila kuyaweka bayana.

Mtindo au tabia ya wanaume kukaa kimya dhidi ya unyanyasaji wanaofanyiwa na wake zao na wakati mwingine kushirikiana na watoto, umepitwa na wakati, hivyo ni wakati mwafaka kwao kupaza sauti pindi wanapokutana na mambo kama hayo ili kuokoa maisha yao na kuwaepusha na madhara yanayoweza kuwapata.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Hili la noti kuchakazwa, daima lisifumbiwe macho

**WIZARA** ya Fedha na Mipango Zanzibar, wiki iliyopita ilieleza kuhusu kuchakaa noti ya Tanzania, kunakofanywa na baadhi ya wananchi, wanapokuwa kwenye sherehe mbalimbali za kijamii.

Wizara hiyo ilieleza kuwa kuchakaa kwa noti hizo, kunatokana na matumizi mabaya kwenye wimbi la sherehe za harusi nchini.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, alikaririwa akiyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi visiwani humo, wakati akijibu swali la mmoja wa wawakilishi aliyetaka kujua matumizi haramu ya noti hizo na hatua zinazochukuliwa kwa mtu anayebainika, anaidhalilisha na kushusha thamani noti hiyo.

Alichosema waziri ni sahihi kabisa, kuwa kuna watu wamekuwa na tabia ya kurusha kwa maharusi noti iwe sakafuni, ukumbini na kwingine kisha kukanyagwa.

Vilevile wako wanaoviringisha noti katika maumbo na kutumika kama mapambo na kuweka kwenye mwili wa mtu wenye jasho na kusababisha kuchakaa na kukosa hadhi yake stahiki.

Siyo hivyo tu, noti hizo pia zimekuwa zikihifadhiwa vibaya na baadhi ya wafanyabiashara wakiwamo wa mkaa na kusababisha kuchakaa kwa kukunjwa, visivyo na kuchafuka masizi kiasi cha kutokuwa na thamani kwa kuanza kuchanika.

Vilevile noti hizo zimekuwa zikichakaa kutokana na wafanyabiashara wa maji kuzihifadhi zikiwa zimelowa baada ya kupokea kutoka kwa wateja.

Mitaani kuna noti, ambazo ziko kwenye mzunguko wa biashara zimechakaa kutokana na wafanyabiashara kukosa umakini katika kuzihifadhi.

> **Siyo hivyo tu, noti hizo pia zimekuwa zikihifadhiwa vibaya na baadhi ya wafanyabiashara wakiwamo wa mkaa na kusababisha kuchakaa kwa kukunjwa, visivyo na kuchafuka masizi kiasi cha kutokuwa na thamani kwa kuanza kuchanika.**

Kati ya noti hizo, zipo ambazo zimekatwa kwenye kona kwa madai kuwa ya kudhibiti kuibwa kwa njia ya mazingaombwe maarufu kama chuma ulete.

Ni ukweli usiopingika kuwa uchakavu huo wa noti, unaipotezea sifa fedha hiyo ya Tanzania, kwa kuwa ni moja ya tunu za taifa letu.

Kinachosikitisha kuwa, vitendo hivyo vinaendelea kukithiri nchini, licha ya kuwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), maofisa wake waandamzi na viongozi wa serikali wamekuwa wakikemea na kuitaka jamii kulinda tunu hiyo.

Jamii inatakiwa kuelewa kwa tabia hiyo ya kuharibu noti na sarafu inatakiwa kukomeshwa kwani ni dharau na dhihaka kwa Serikali.

Ieleweke kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ina kifungu kinachoainisha kuwa ni kosa la jinai kwa kutumia vifungu na kanuni za adhabu, kama ilivyorejewa mwaka 2002.

Hivyo, mwananchi atakayebainika akitenda kosa hilo iwe kwa bahati mbaya au makusudi akamatwe na kushtakiwa kwa kosa la jinai na kuhukumiwa kutumikia kifungo jela, ili kukomesha tabia hiyo ambayo imekuwa ikiota mizizi siku hadi siku.

Watanzania ieleweke kwamba serikali inatumia fedha nyingi, kwa ajili ya kuchapisha noti mpya na kutengeneza sarafu, hivyo ni jukumu letu kuisadia kupunguza gharama kwa kuokoa fedha ambazo zinatumia kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa manufaa yetu sote.

Miradi hiyo ya jamii ni pamoja na kusogeza huduma ya maji, umeme, elimu, afya na ujenzi wa barabara, madaraja na mingine mingi.

## KKKT waadhimisha Uhuru kwa kuombea amani nchini

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WAUMINI wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Mirerani, Jimbo la Arusha Mashariki, Dayosisi ya Kaskazini Kati, Wilaya ya Simanjiro mkoani hapa, wameungana na wenzao kuombea amani ya nchi wakati wa Maadhimisho ya Miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika.

Maombi hayo yalifanyikia baada ya Mchungaji wa KKKT, Usharika huo, Loishiye Godson Laizer kuongoza matembezi hayo kuanzia kanisani hapo hadi ukuta unaozunguka migodi ya madini ya Tanzanite iliyopo mji mdogo wa Mirerani.

Mchungaji Laizer, alisema lengo ni kuombea amani ya nchi, viongozi na jamii ni kuifanya Tanzania iendelee kuwa salama. "Tumekutana kwa ajili ya maombi baada ya matembezi ya amani na tunawapongeza wote waliojitokeza, tunamshukuru Mungu kwa kusimama na sisi hadi tukamaliza jambo hili," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea matembezi hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji huo, Isack Mgaya, aliwapongeza viongozi na waumini hao na wengine kwa uamuzi huo.

Mgaya, alisema amemuwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Fakii Lulandala kupokea mapokezi hayo na kushiriki ibada ya maombi ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku hiyo ya Uhuru ambayo hufanyika Desemba 9, kila mwaka.

"Watu wa imani mbalimbali tuendelee kuliombea Taifa letu na Rais Samia Suluhu Hassan aendelee kuongoza kwa amani, utulivu na uadilifu," alisema.

Kwa upande wake, Mchungaji wa Kanisa la Anglikana Mirerani, Amon Nzikobankunda, alisema wameshiriki kuliombea Taifa na viongozi wake ili amani izidi kudumishwa katika jamii.

# EPZA: Diplomasia uchumi ya Samia yavutia wawekezaji wengi kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), imesema kuwa diplomasia ya kiuchumi ya Rais Samia Suluhu Hassan, imekuwa kichocheo muhimu katika kuvutia wawekezaji wa kimataifa kuja Tanzania.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe, alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam alipokutana na ujumbe kutoka Chemba ya Biashara kutoka Dubai (Dubai Chamber of Commerce), ambao wamekuja kutafuta fursa za uwekezaji.

"Tanzania sasa inatambulika kama lango la wazalishaji wanaolenga masoko ya Afrika na duniani kote," alisema, akitaja ziara hiyo ya hadhi kubwa kama matunda ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan. Itembe alihakikishia ujumbe wa Chemba ya Biashara ya Dubai kuhusu usalama wa uwekezaji wao Tanzania.

Alisisitiza kuwa uhusiano mzuri wa kidiplomasia na ushirikiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na nchi mbalimbali unafanya nchi kuwa kivutio bora cha uwekezaji.

Aidha, Tanzania inashiriki katika Eneo la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA), ambalo linatoa fursa ya kuuza bidhaa zilizo kwenye Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZs) katika soko la Afrika bila kodi na vikwazo vya kibiashara.

Aliwataka wanachama wa Chemba ya Biashara ya Dubai kuchukua fursa ya uwekezaji kwa wakati mwafaka.

Aliwaambia kuwa Tanzania imeweka mkazo katika kutenga maeneo mengi kwa ajili ya kuanzisha SEZs ikiwa ni pamoja na kuweka miundombinu wezeshi, mfano Bagamoyo SEZ, ambalo peke yake linatarajiwa kuwa na viwanda zaidi ya 2,000.

**"Kwa ziara hii na nyingine za wafanyabiashara kutoka nje, EPZA inalenga kuongeza ushindani wake katika kuvutia wawekezaji wa viwanda kutoka nchi mbalimbali, ikiwamo za Kiarabu...**

Mengine ya kipaumbele ni Dodoma, Tanga, Kwala na Kigoma, ambayo EPZA imetenga maeneo makubwa kwa ajili ya maendeleo ya viwanda.

Alisema sekta binafsi inakaribishwa kuwekeza katika miundombinu na kujenga viwanda kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

"Kwa ziara hii na nyingine za wafanyabiashara kutoka nje, EPZA inalenga kuongeza ushindani wake katika kuvutia wawekezaji wa viwanda kutoka nchi mbalimbali, ikiwamo za Kiarabu na hivyo kuleta matokeo chanya kwa ukuaji wa uchumi wa Tanzania," alisisitiza.

Aidha, ziara ya ujumbe huo kutoka Dubai ni uthibitisho wa kukubalika kimataifa kwa programu za Maeneo Maalum ya Uzalishaji (EPZ) na Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ).

Akielezea ajenda ya ziara hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa EPZA alisema ilikuwa na lengo la kuimarisha ushirikiano uliopo kati ya EPZA na Chemba ya Biashara ya Dubai.

Ujumbe huo pia ulitaka kujua zaidi fursa za uwekezaji zinazopatikana katika SEZs za Tanzania.

Rais wa Chemba ya Biashara kutoka Dubai na kiongozi wa ujumbe, Mohammad Ali Lootah, alisema biashara kati ya Tanzania na Dubai imekua kwa kiasi kikubwa ambao sasa umefikia Dola za Kimarekani bilioni 2.7.

Ongezeko hilo linachangiwa na uhusiano mzuri wa biashara kati ya Tanzania na UAE, ulioimarishwa na uwekezaji unaoendelea katika sekta ya bandari za Tanzania. Kwa kuzingatia uhusiano mzuri kati ya Tanzania na Dubai, Lootah, alisema wawekezaji wengi wanavutiwa kuchunguza fursa za uwekezaji nchini Tanzania kupitia Maeneo Maalum ya Kiuchumi.

Alisema EPZA inapaswa kutarajia kuongezeka kwa idadi ya wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda watakaotaka kutambua fursa katika sekta ya viwanda ya Tanzania na zaidi.

CRDB BANK

**Benki ya CRDB PLC** inatangaza kupotelewa na kadi za magari yafuatayo kama zilivyotolewa na TRA;

**T 883 ECY, T 359 DAY, T 522 DEF, T 530 DSP, T 469 BET, T 345 DWE, T 547 BDU, T 822 DEE, T 900 DGH, T 671 CAM, T 521 DEF, T 867 DGH, T 849 DHN, T 591 ECX, T 590 DCW, T 855 DGH, T 863 DGH, T 858 DGH, T 114 DWB, T 457 BGA, T 588 ECX, T 864 DGH, T 983 DGH, T 107 EDV, T 150 DYW, T 150 EDB, T 150 DXW, T 956 DXB, T 356 DAY, T 354 DAY, T 664 CPJ, T 874 DTV, T255 DBW, T 343 DAY, T 343 BRQ, T 341 CPK, T 492 BDU, T 350 DBW, T 207 EDP, T 522 BSS, T 874 CMR, T 348 DBW, T 585 ECX, T 320 DEF, T 516 DEF, T 697 EBH, T 936 EBH, T 212 EDP, T 285 CBS, T 119 EDV, T 767 EGD, T 859 DGH, T 439 BDU, T 865 DGH, T 247 DHA, T 496 BDU, T 435 DBW, T 869 DGH, T 673 CPJ, T 351 DGH.**

Taarifa imetolewa kituo cha polisi Kwa kumbukumbu namba.

**PHQ/DAR/KIN/269663/2024**

**PHQ/DAR/KIN/269677/2024**

**PHQ/DAR/KIN/269669/2024**

**PHQ/DAR/KIN/269665/2024**

# TPA kuongeza magati mawili kurahisisha upakuaji mizigo

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), iko kwenye mpango wa kujenga magati mengine mapya mawili hivyo kufanya kuwa na magati 12 katika bandari ya Dar es Salaam hali ambayo itachochea ukuaji wa uchumi wa nchi.

Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, ilisema jana kuwa asilimia 95 ya shehena zote zinazoingia nchini hupitia bandari ya Dar es Salaam, hivyo wameona umuhimu wa kuongeza magati.

"Kuongezeka kwa magati hayo kutachochea ongezeko la wateja wa ndani ya nchi sambamba na nchi jirani zinazotuzunguka zikiwamo Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Zambia na Malawi," alisema Mbossa.

Alisema maboresho makubwa na uwekezaji unaoendelea kufanywa katika Bandari ya Dar es Salaam yamekuwa kivutio kwa mataifa mbalimbali ya Afrika, Asia na Ulaya kwa kuwa wamekuwa wakija kuangalia na kushuhudia utendaji kazi wake na uwezekano wa kuanza kufanya kazi nao.

Taarifa hiyo ilisema Rais Samia Suluhu Hassan katika uongozi wake wa miaka mitatu ameiboresha bandari ya Dar es Salaam kwa kuruhusu wawekezaji DP World ambaye anasimamia gati namba 4 mpaka 7 na Adan International Ports Holding ambaye anasimamia gati namba 8 mpaka 11.

Katika kukuza ushirikiano na nchi za jirani na kuendelea kuzishawishi kuendelea kutumia bandari ya Dar es Salaam, Mboasa alisema tayari wameshafungua ofisi za TPA Malawi na Zambia, kwa lengo la kuwafikia wateja moja kwa moja.

**"Kuongezeka kwa magati hayo kutachochea ongezeko la wateja wa ndani ya nchi sambamba na nchi jirani zinazotuzunguka zikiwamo Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo,**

"Ujenzi wa haya magati pamoja na ufunguzi wa ofisi zetu katika nchi tajwa utasaidia sana kupunguza foleni kwa wateja pia kuongeza idadi ya wateja. Awali meli ikishafika katika bandari ya Dar es Salaam ilikuwa inachukua siku 30 mpaka kushusha shehena lakini kwa sasa inachukua siku nne mpaka tano tu," alisema.

Mbossa alisema kwa sasa bandari ya Dar es Salaam hupakua makontena 100,000 kwa mwezi kutoka makontena 70,000 awali na ongezeko la ujenzi wa gati utasababisha kushusha idadi kubwa zaidi ya kontena kwa mwezi.

Alisema licha ya maboresho yanayofanywa na TPA, wanaendelea kuboresha mfumo wa malipo wa kidijitali ambao utamwezesha mteja kufanya miamala popote pale alipo.

Kuhusu kuchangia pato la taifa, Mbossa alisema TPA inachangia zaidi ya asilimia 7.3 kwa mwaka lakini lengo ni kuhakikisha sekta hiyo inachangia asilimia 15 ya pato la taifa.

Alisema hivi karibuni Umoja wa Ulaya (EU) ulitembelea bandari ya Tanga na kuipongeza serikali ya Tanzania kwa uwekezaji mkubwa katika miradi mbalimbali na maboresho ya bandari yenye lengo la kuongeza ufanisi na kuwezesha biashara kufanyika kwa urahisi.

Mbosa alisema TPA ilitembelewa na Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe de Boer na ujumbe wake katika bandari ya Dar es Salaam ambao pamoja na mambo mengine, aliipongeza serikali kwa kuendelea kuweka mazingira mazuri ya biashara.



Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka (kulia), akitoa pole na kumkabidhi rambirambi Stella Kaaya, mtoto wa mwanamazingira maarufu wa mji mdogo wa Mirerani, Amos Kaaya aliyefariki dunia hivi karibuni na kuzikwa mtaa wa Kairo, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mthamini mkuu ahimiza uadilifu utendaji kazi

**Na Munir Shemweta**

MTHAMINI Mkuu wa Serikali, Evalyne Mugasha, amewataka wathamini nchini kuwa makini na waadilifu na kufanya kazi kwa uadilifu ili kuepuka migogoro inayotokana na kazi zao. Mugasha aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wathamini pamoja na warasimu ramani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wanaopata mafunzo kwa ajili ya uandaaji vitalu vya thamani ya ardhi yaliyoandaliwa na wizara kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP) yanayofanyika jijini Dar es Salaam.

"Hakuna uthamini mbaya bali cha msingi ni kuwa makini na kazi zenu na kuhakikisha mnafanya kazi kwa umakini na uadilifu huku mkizingatia sheria na miongozo ya taaluma zenu ili kuepuka malalamiko dhidi yenu," alisema.

Mugasha alisema mafunzo wanayoyapata watumishi hao wanatakiwa kuyachukulia kwa umakini mkubwa kwa kuwa yanawapeleka kwenye mfumo wa kidijitali (e-ardhi) ambao alisema kwa kiasi kikubwa utaondoa dhana ya udanganyifu unaoweza kutokea wakati wa kazi zao.

Kwa mujibu wa Mthamini Mkuu, watumishi wanaochukua mafunzo hayo wanatakiwa kubadilika kiutendaji huku akiwataka kutokubali kubadilishwa na badala yake wabadilike wenyewe na kufanya kazi kwa kuzingatia maadili kwa kuwa uthamini unagusa watu wengi. Mratibu wa Mafunzo hayo, Baraka Mollel, alisema mafunzo hayo ni njia mojawapo ya kuwajengea uwezo wathamini na warasimu ramani wa wizara ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi hasa kipindi hiki ambacho wizara imeboresha mifumo na kuwa ya kidijitali.

Kwa mujibu wa Mollel, vitalu vya thamani ya ardhi vitajumuishwa kwenye mfumo wa e- ardhi utakaowezesha ulipaji tozo mbalimbali zikiwamo kodi ya ardhi, kodi ya ongezeko la thamani na tozo zingine zinazotokana na thamani.

"Mafunzo ya uandaaji vitalu vya thamani kwa wathamini na warasimu ramani yatawezesha kujumuishwa kwa vitalu kwenye mfumo wa e-ardhi na kuwezesha ulipaji tozo mbalimbali ikiwemo kodi ya ardhi na tozo zingine zitokanazo na thamani," alisema.

Mollel aliongeza kuwa mafunzo hayo yatasaidia katika utekelezaji wa shughuli za uthamini kama vile rehani, uhamishaji milki na uthamani kwa ajili ya mahitaji mbalimbali ya serikali.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeanza matumizi ya mifumo ya kidijitali (e-ardhi) na hivi karibuni wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi,

Waziri wake, Deogratius Ndejembi, aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi kuhakikisha wanatumia mfumo huo katika maeneo ambayo mfumo huo umeanza kutumika.

Mfumo wa e-ardhi umeanza kutumika kwenye maeneo mbalimbali nchini kama vile Dodoma, Arusha, Tabora katika halmashauri ya Nzega, Pwani halmashauri ya Chalinze na manispaa ya Shinyanga na Kahama mkoani Shinyanga.

# Waziri: WHI imeleta mapinduzi katika umiliki nyumba kwa watumishi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amesema Watumishi Housing Investments (WHI) imefanya mambo makubwa kwa watumishi kumiliki nyumba za makazi.

Amesema tangu kuanzishwa kwake, imeleta mapinduzi makubwa kwa watumishi wa umma kumiliki nyumba bora kwa masharti nafuu, hatua inayolenga kuboresha hali ya maisha na kuongeza ufanisi kazini.

Simbachawene alisema hayo juzi katika eneo la nyumba zilizojengwa na WHI, Njedengwa jijini Dodoma, wakati akimkaribisha Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kuzindua Mpango wa Makazi kwa Watumishi wa Umma.

Alisema WHI imetekeleza mpango wa makazi kwa watumishi wa umma nyumba 1,006 katika mikoa 19 nchini lengo likiwa ni kutatua changamoto ya makazi inayowakabili watumishi hao, hususan wa kipato cha chini.

Waziri Simbachawene alisema mpango huo ulibuniwa ili kuwapa nafuu watumishi kumiliki nyumba ikizingatiwa kuwa katika kipindi cha nyuma, haikuwa rahisi kwa watumishi hao kumiliki nyumba kutokana na kampuni nyingi zinazojihusisha na ujenzi wa nyumba kujiendesha kibiashara kwa lengo la kupata faida.

Alisema shabaha kubwa ya WHI ni kujenga nyumba vijijini kwa ajili ya kuwawezesha watumishi wa kipato cha chini, wakiwamo walimu na wauguzi kumiliki nyumba na kujenga maeneo ya mijini ili kuwasaidia watumishi wenye kipato cha chini na ajira mpya kuacha kupanga nyumba mbali na maeneo ya kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC), Augustine Holle, alisema WHI ni taasisi ambayo imekuwa ikijenga nyumba zinazouzika tofauti na taasisi zingine kutokana na kujenga nyumba kulingana na kipato cha wateja ambao ni watumishi wa umma.

"WHI ni taasisi makini ambayo imejikita kurahisisha umiliki wa nyumba kwa watumishi wa umma kuwa urahisi na endelevu," alisisitiza.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa WHI, Dk. Fred Msemwa, alisema suala la makazi kwa watumishi wa umma ni jambo lisiloepukika kwa kuwa linachochea ufanisi wa kazi kwa Watumishi hao.

Alisema tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo, wamekuwa wakifanya jitihada za kujenga nyumba za watumishi kwa bei rahisi ili kuwawezesha kumiliki nyumba kwa kuzinunua kwa bei rahisi.

"Kwa mara ya kwanza haikuwa rahisi. Nyumba zilizojengwa licha ya kuwalenga watumishi walikuwa hawawezi kuzinunua kutokana gharama kuwa juu lakini kwa sasa watumishi wamekuwa wakizifurahia," alisema.



# Madiwani waicharukia TARURA, DC awapoza

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MADIWANI wa Halmashauri ya Jiji la Arusha wameucharukia uongozi wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Arusha mkoani hapa kwa madai ya kushindwa kukarabati barabara na kujenga vivuko katika baadhi ya kata.

Ni baada ya halmashauri hiyo kutenga Sh. milioni 28 kwa kila kata kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika kikao cha baraza la madiwani kilichofanyika juzi, walisema kwa zaidi ya miezi mitatu tangu wapokee fedha hizo, TARURA hawajafika kwenye barabara hizo na wananchi wanaendelea kupata adha ya usafiri.

Walisema adha hiyo inatokana na baadhi ya barabara kwenye kata kutopitika kutokana na ubovu.

Diwani wa Lemara, Naboth Silasie, alisema walikabidhiwa barua za mkataba kutoka halmashauri hiyo Septemba 3, mwaka huu kwa ajili ya kutengeneza barabara hizo, lakini mpaka sasa hakuna mkandarasi aliyefika kwenye kata yake.

"Kitengo cha manunuzi, mhandisi wa ujenzi malalamiko yenu ni mengi mnatugombanisha na wananchi kwa sababu madiwani wengi walishafanya mikutano ya hadhara na kuwaeleza kila kata imepatiwa shilingi milioni 28 za ukarabati wa barabara," alisema Silasie.

Diwani wa Olasiti, Alex Mart, alisema hali ya barabara katika kata yake ni mbaya, wananchi wanapata adha ya usafiri licha ya Sh. milioni 28 kupelekwa kwenye kata yake, lakini mpaka sasa TARURA hawajapeleka mkandarasi.

"Kwenye kata zetu wananchi hawatuelewi hali ni mbaya hasa kipindi hiki cha mvua licha ya fedha kutengewa," alisema Mart na kuongeza:

"Tunamuomba mkuu wa wilaya atuondolee Meneja wa TARURA wa wilaya kwa kuwa ameshindwa kusimamia majukumu yake kuhakikisha barabara zinapitika muda wote." Diwani wa Ngarenaro, Isaya Doita, alisema asilimia kubwa ya barabara katika kata ni zina lami na kuna kata hali ya barabara ni mbaya.

Doita, alisema anaamini ofisi ya mhandisi wa ujenzi na kitengo cha manunuzi wanakwamisha zisikarabatiwe kwa wakati.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkuu wa Wilaya hiyo, Felician Mtahengerwa aliagiza uongozi wa halmashauri hiyo kuwasilisha taarifa ya watumishi wanaokwamisha ujenzi wa barabara hizo ofisini kwake ili wachukuliwe hatua.

Mtahengerwa, vilevile aliahidi kukutana na meneja wa TARURA wa wilaya hiyo ili kujua sababu za kukwama kwa ukarabati wa barabara hizo.

"Tulitenga fedha na kuweka msisitizo wa kujenga mifereji ili kuokoa barabara zetu ikiwa ni pamoja na kukarabati ambazo haziko katika hali nzuri miezi mitatu iliyopita, mpaka sasa hakuna kilichofanyika na mvua zimeanza kunyesha," alisema na kusisitiza kuwa:

"Nataka nipate taarifa za nani anakwamisha ujenzi wa barabara kwa sababu kila kata imepata shilingi milioni 28." Aliwaasa madiwani hao kuwa muda wao uliobaki ni mchache na kwamba wakicheka na nyani watavuna mabua.

" Acheni mazoea na watumishi wa Halmashauri ya Jiji ni kwa muda mrefu sasa hakuna miradi inayotekelezwa licha ya fedha kutengwa na nyingine kupelekwa kwenye akaunti za kata," alisema.

Mtahengerwa alihoji kuhusu Sh.milioni 450 zilizotengwa kuweka taa za barabarani kutokana na maeneo mengi ya jiji hilo kuwa giza.

"Kaimu Mhandisi wa ujenzi nataka kujua ziko wapi shilingi milioni 450 tulizotenga kuweka taa barabarani kwa sababu mji bado ni giza na hivi karibuni tulipopata ugeni wa marais nane tulilazimika kutafuta fedha za dharura kuweka taa wakati fedha mnazo," alisema.

Akijibu malalamiko ya madiwani hao, Meneja wa TARURA wa Wilaya hiyo, Albert Kyando, alisema walipeleka mahitaji ya kukarabati barabara na kujenga vivuko ofisi ya halmashauri hiyo na wakandarasi, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea.

"Sisi tuko tayari kwa kazi na mahitaji yote tuliyawasilisha ili wayafanyie kazi lakini mpaka sasa hatujapata majibu," alisema Kyando.


CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30821 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

ECN GLOBAL SERVICES LTD .... ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Managing Director, ECN Global Services Limited of Kigogo First Inn Street / Mburahati Junction, Kinondoni Municipality, DSM City

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of Decemba 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 28 day of Novemba 2024

RESIDENT MAGISTRATE COURT KIVUKONI/KINONDONI, DAR ES SALAAM

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

218295802

CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30826 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

NASSOR AHMED SALEH .... ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Nassor Ahmed Saleh of Plot No. 9, Block F, Narung'ombe Street, Kariakoo Area, Ilala Municipality, DSM

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 28 day of November 2024

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

218295802

CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30815 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

CENTURY PROPERTIES LIMITED .... ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Managing Director, Century Properties Limited of Plot No. 251/41, Kinondoni Area, Along Morogoro Road, Kinondoni Municipality, DSM City

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 28 day of November 2024

RESIDENT MAGISTRATE COURT KIVUKONI/KINONDONI, DAR ES SALAAM

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

218295802

CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30838 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

MOHAMED ABDU MAJID .... ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Mohamed Abdu Majid of Plot No. 589, Block 40, Hananasif Area, Kinondoni Municipality, DSM City


WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 28 day of November 2024

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

218295802



## HABARI KANDA YA ZIWA

# 'Yaya' ajimaliza kwa kitanzi chumbani

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

MFANYAKAZI wa ndani aliyefahamika kwa jina moja tu la Modesta (17), Mkazi wa Kata ya Makoko Manispaa ya Musoma mkoani Mara anadaiwa kujiua kwa kujinyonga kamba ya kufungia mbuzi kwenye paa chumbani kwake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Pius Lutumo alisema kuwa tukio hilo lilitokea Desemba 10, mwaka huu majira ya asubuhi katika Mtaa wa Zanzibar Makoko.

"Katika tukio hili la binti huyu alikuwa anafanya kazi za ndani alikutwa akiwa amefariki dunia akidaiwa kujinyonga kwa kutumia kamba ya kufungia mbuzi, mwili wa marehemu ulikutwa umening'inia kwenye kenchi ya paa la chumba alichokuwa analala," alisema Lutumo.

**Hata hivyo, alisema inahofiwa kuwa huenda chanzo cha kifo hicho ni kutokana na msongo wa mawazo kumkumba mfanyakazi huyo wa kazi za ndini.**

Alisema uchunguzi kuhusiana na mazingira ya kifo hicho bado unaendelea na kwamba utakapokamilika familia itakabidhiwa mwili kwa ajili ya mazishi

Hata hivyo, alisema inahofiwa kuwa huenda chanzo cha kifo hicho ni kutokana na msongo wa mawazo kumkumba mfanyakazi huyo wa kazi za ndini.

Kamanda huyo aliwataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi wanapokutwa na msongo wa mawazo bali watafute ushauri kwa watu wa umri mkubwa wenye busara, viongozi wa dini na wataalamu wa masuala ya ushauri nasaha waliopo katika maeneo mbalimbali wilayani hapa na si kuchukua uamuzi wa kujiua kwa kuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria za nchi.




Timu ya Wanasheria wanawake wa Mkoa wa Shinyanga, wametoa msaada wa mashine ya kupumulia watoto njiti, katika Hospitali ya Rufani ya mkoa huo, juzi. Kulia ni Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, Ruth Massam akikabidhi mashine hiyo kwa niaba ya timu hiyo kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Luzila John.
**PICHA: MARCO MADUHU**

## 'Waandishi fichueni watumishi wahalifu'

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

WAANDISHI wa habari wilayani hapa Mkoa wa Mara wameombwa kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola kwa kufichua uhalifu unaofanywa na baadhi ya watumishi wa umma ili kujenga nidhamu nchini.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Mratibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu wilayani hapa, Bonny Matto wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu duniani.

Matto, alisema waandishi kupitia taaluma yao wanapaswa kutoa elimu ya sheria kwa umma kuhusiana na ulinzi wa haki za binadamu ili jamii iwafichua wahalifu.

"Waandishi wanatakiwa kuacha kuogopa kuripoti mapambano dhidi ya uvunjifu wa amani, utekaji na uhalifu mwingine unaovunja haki ya kuishi ya wananchi," alisema

Aliishauri serikali kuwapatia waandishi ulinzi kama mabalozi wa kuuhabarisha umma kwa kuwa wanaotoa taarifa za uhalifu wa makosa wanayoshuhudia yakitendeka katika jamii inayowazunguka.

Matto, alisema wanahabari hawapaswi kuogopa kufichua maovu kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu kuwa hakuna mtu atakayeteswa au kutendewa vitendo vya kikatili, kinyama, kudhalilisha au kuadhibiwa.

"Haki za binadamu lazima ziheshimiwe na kila mtu kila siku na kila mahali kama msingi wa jamii unaopaswa kufurahiwa na wanadamu wote bila kujali dini, rangi, kabila, jinsia na hadhi zao," alisema.

# Jela miaka 30 kwa kumbaka mtoto

**Na Daniel Limbe,** CHATO

MAHAKAMA ya Wilaya ya Chato mkoani Geita, imemhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 jela, Lucas Albogast (33) baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 14.

Awali Mwendesha Mashitaka kutoka Ofisi ya Mashitaka ya Wilaya hiyo, Mauzi Lyawatwa alidai kuwa Machi 3, mwaka huu, usiku katika Kijiji cha Rwantabe Kata ya Bwanga, mshtakiwa huyo alivunja mlango kwa kutumia jiwe maarufu fatuma na kuingia ndani kwenye nyumba alimokuwa amelala mtoto huyo na kumuweka chini ya ulinzi.

Lyawata, alidai kuwa mshtakiwa huyo alimuweka chini ya ulinzi mtoto huyo baada ya kumkuta amelala sebuleni na kuwafungia wazazi ndani ya chumba chao kwa komeo.

Alidai mshtakiwa huyo kwa kukusudia kufanya uhalifu huo, alianza kutoa amri kwa wazazi wa mtoto huyo kutoa fedha haraka na kutokomea kusikojulikana baada ya kudai hawana fedha.

Lyawatwa alidai mshtakiwa huyo alimpeleka mtoto huyo porini na kumlazimisha kufanya naye mapenzi. Aliiomba mahakama huyo kumpa adhabu kali mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo ya ubakaji.

Awali mahakama hiyo ilipitia ushahidi uliowasilishwa mbele yake, ikiwemo jiwe lililotumika kuvunja mlango 'Fatuma', fomu maalumu ya matibabu kutoka polisi (PF3) na fomu maalumu ya utambuzi wa mtuhumiwa.

Vilevile, ilisikiliza na kupitia maelezo ya mashahidi watano wa upande wa mashtaka, akiwemo daktari, ungamo na onyo la mlinzi wa amani.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Erick Kagimbo, alimpatia mshtakiwa huyo fursa ya kujitetea ili apunguziwe adhabu kwa kuwa ni haki yake.

Mshtakiwa huyo aliiomba mahakama hiyo kusamehewa kwa madai kuwa ana familia yenye watoto watatu. inayomtegemea.

Hakimu Kagimbo, alisema ushahidi uliotolewa na upande wa mashitaka na utetezi katika kosa la kwanza la unyang'anyi wa kutumia silaha, mahakama hiyo inamwachia huru.

Alisema kwa kosa la pili la ubakaji, alisema ushahidi uliowasilishwa mahakamani hapo umetosha kuishawishi mahakama hiyo pasipo kuacha shaka mshtakiwa alitenda kosa hilo kwa kukusudia na kumhukumu kiifungo hicho jela. Hata hiyo, alisema mshtakiwa huyo anaweza kukata rufaa kupinga hukumu hiyo ndani ya siku 30 tangu ilipotolewa na mahakama hiyo.



Ukurasa 12

**MIAKA 64 YA UHURU....**

**Simulizi za mafanikio, magumu ya uchumi wa kijamaa na kitendawili cha kuwapo kwake**



Ukurasa 13

Kwa utangazaji huu hakika tunavuna mabua



Ukurasa 14

**Zama za Dk. Samia na Ujamaa katika uchumi – siasa zinavyosafiri nchini**


# BUFE

IJUMAA DESEMBA 13, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


# Kikundi kinamama wamechanga Sh.500 kila mmoja kwa siku, wanunua basi

• Dereva mwanamke; dhamira kuu matano

**Na Halfani Chusi**

HAYAWI hayawi sasa yamekua! Ni baada ya Umoja wa Vikundi vya Ujasiriamali Kivule (UVUKI) kuchangishana fedha hadi kufanikisha kununua basi dogo la abiria 25, aina ya Toyota Coaster.

Ni kikundi chenye maskani yake Kivule, wilayani Ilala, Dar es Salaam, kikisimamiwa na Shirikisho la Vikundi vya Ujasiriamari Tanzania (SHIVUTA) chini ya Mkurugenzi wake Andrew Koti, kuanzia mwaka jana kilifanikiwa kuchanga na kukusanya zaidi ya milioni 80.

Hata hivyo, lengo lake ni kufikisha mabasi kama hayo matano ifikapo mwaka 2025, mikakati ya kuagiza nyingine inaendelea sasa. Siku ya uzinduzi wa mradi huo, waalikwa walishuhudia nderemo za wanakikundi hao wapatao 600.

Mvuto mwingine ukawa, kuchaguliwa mwananmke kuwa dereva wa gari hilo, aliyesomeshwa udereva na kikundi, ili awe mkamilifu barabarani.

Mkurugenzi wa Shivuta, Andrew Koti, anatamka: "Tunamuomba Rais Samia atusaidie kutununulia Coaster (basi) moja, tunai mani naye tunajua ni msikivu atatusikia..."

Anasema kazi ya shirika lake ni kusimamia vikundi vya kuweka na kukopa, na mradi wa basi hilo uko kuwarahishia katika shughuli mbalimbali.

"Katika maeneo mengine ninayoyasimamia kuna miradi mingine, lakini kwa Kivule wamechagua Coaster, ili iwe rahisi kwa ajili kurahisisha shughuli za maendeleo" anasema Koti

Anasema wajumbe 600 wa umoja huo, wameshiriki pamoja kuchanga na ikapatikana Sh milioni 80 zilizowezesha kupatikana basi hilo.





Katibu Tawala Wilaya ya Ilala, Flora Mgonja (kulia), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa basi la kikundi cha Uvuki. Kushoto ni Mlezi wa kikundi, pia mshindi wa mashindano Miss Word Tanzania, mwaka 2021, Juliana Lugumisha. **PICHA: HALFANI CHUSI**

**DAS ILALA**

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya Ilala, Edward Mpogolo, Katibu Tawala wake, Flora Mgonja, anawapongeza wana kikundi hicho kutimiza ndoto yao.

Anaitaja kuwa faraja kwa uongozi wa wilaya hiyo, kuona kuna vikundi vinavyopambana kujiinua kiuchumi, akisifu tafsiri yake, itainua uchumi wa nchi kwa pamoja.

"Leo nimezindua Coaster moja kubwa, ambayo ilikuwa ndoto yao na nyingine tano, zinakuja wamemuunga mkono Rais Samia, katika ile dhana ya uwezeshaji wanawake kiuchumi.

"Hawa ni wajasilimali, lakini ni kikundi cha watu tofauti na leo tuko hapa tukiwashuhudia Uvuki. Lakini, kubwa zaidi wametengeneza ajira na kilichonifurahisha aliyepewa rukhsa ya kuliendesha gari hilo ni mwanamke.

"Ninaendela kuwaambia wapendane, kwa sababu umoja unahitaji ushirikiano na sisi tunajivunia kuwa na watu wenye maono ya mbali" akatamka na kupokewa kwa shangwe ya wanakikundi waliokuwa na sare maalum.

Frola, anatoa wito kwao Wana Ilala, kuiga mfano huo, kutumia fursa. Alipoulizwa na Nipashe, kuhusu ombi lao la msaada wa basi kwa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan kupitia kwake, akasema amepokea taarifa hizo na atazifikisha panapohusika.

Mlezi wa Kikundi, Juliana Lugumisa, anasema basi walilolinunua itawasaidia kupata nyingine, akisisitiza juhudi za awali ni ngumu, lakini tayari wameanza kufanikiwa.

Juliana anarejea hoja hiyo, akitamka: "Tunamuomba mama yetu (Rais), atusaidie kupata kosta nyingine, hizo tatu zitakazobaki tutapambana kwa juhudi zetu wenyewe mpaka tufikie malengo."

Juliana, mwenye wasifu mwingine; mshindi wa mchuano wa warembo inayojulikana Miss World Tanzania, 2021, anawasisitiza wanakikundi hao kuendelea kufanya kazi kwa bidii.

"Tumeanza na Coaster moja! Siku zote mwanzo huwa mgumu, lengo ni kufikia tano na tayari moja tumeshamuomba Rais Samia atusaidie. Nina hakika atasikia kilio chetu na kutuunga mkono" anasema Juliana, huku akipokewa kwa shangwe ya wajumbe wa kikundi.

Pia kikundi kinatajwa kujiweka katika nafasi ya kupata mikopo ya halmashauri inayotolewa na serikali. Mara kadhaa, serikali imekuwa ikisistiza wanaohitaji mikopo ya kiserikali, wajiunge katika vikundi, iwe rahisi kuipata na kutambuliwa kirahisi.

Wanakikundi hao waliendesha harambee ya kuchanga mpaka kupatikana kiasi hicho cha fedha; wakichanga Sh. 500 kila siku, ambayo ni Sh 15,000 kila mwezi kwa mwanachama.

**WANAFUNZI WASAIDIWA**

Katika hatua nyingine, Kikundi hicho, kiliungana na Taasisi ya Mwalimu Ng'ara Foundation, inayosaidia wanafunzi wanaokosa mahitaji muhimu shuleni kutokana na ugumu wa maisha.

Mara hii wanafika katika Shule ya Msingi Ilala Boma iliyoko jijini Dar Nipashe ikiwa shuhuda, wanafunzi wa shule hiyo wamepewa madaftari na mahitajiya kuandikia.


**INAENDELEA UK.14**

UCHUMI

MIAKA 64 YA UHURU WA NCHI...

# Simulizi za mafanikio, magumu ya uchumi wa kijamaa na kitendawili cha kuwapo kwake

**Na Peter Orwa**

WIKI hii Watanzania wanasherehekea miaka 64 ya uhuru wa nchi yao. Ndani ya matofali yaliyowajengea uhai wa kujitegemea, iko siasa ya Ujamaa waliodumu nayo kama nadharia, falsafa, pia sehemu ya miundombinu inayohitajika.

Kwa kina, ndani ya miaka 21; 1964 hadi 1985, Watanzania wamedumu kuwa maswahiba wa kiitikadi wa dola kuu ya Mashariki wakati huo, Muungano wa Jamhuri ya Kisovieti (USSR), hata China na nchi za Ulaya Masharikiu.

Hata hivyo, haikubaki mbali katika unasaba na nchi za Magharibi, hasa Uingereza, kiongozi wa Jumuiya ya Madola ambako nchi inapatikana kuwa koloni lake.

Rais mwasisi, Julius Nyerere na chama chake TANU wakaamua kuchukua njia Ujamaa, akiamini ni rahisi kuwajenga kimaisha wananchi wake, hali kadhalika rahisi kuwafikia kimaendeleo katika mambo ya msingi.

Hiyo inatokana na kanuni ya Ujamaa, njia kuu za kiuchumi, maendeleo zinasimamiwa na serikali, ambayo nayo inawajibika moja kwa moja kuwahudumia, mfano katika mahitaji ya kijamii kama tiba na elimu, pia kuwawezesha kiuchumi kama vile kushiriki kilimo.

Mfumo wa kijamaa ulianza kutekelezwa kwa kina nchini kuanzia mwaka 1964, ikiwa sehemu ya maamuzi makuu kitaifa inayojumuisha: Muungano wa Tanganyika na Unguja; kuundwa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ); Kupitishwa Mpango Mkuu wa Kwanza Maendeleo ya Nchi; Tanzania kutangazwa rasmi siasa ya chama kimoja; TANU kwa Tanzania Bara na Afro Shiraz (ASP) visiwani.

Kihistoria, kuna mengi ya mageuzi kupitia mipango kijamii miaka mitano kila moja (1964-69) na 1969 hadi 1974, ikiwamo kuundwa mashirika ya umma, utititiri wa viwanda, shule, Tanzania kuweka rekodi kimataifa katika mapinduzi kusoma na kuandika.

Ndani yake kuna maamuzi makuu kama: Azimio la Musoma (1974) la elimu na Azimio la Iringa (1972) na ajenda kilimo.

### MAGEUZI 1985

Ilipotimu mwaka 1985 kulikuwapo mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa nchini. Taifa lilirejea mfumo huria uliokuwapo miaka 21 kabla, kisiasa hata kuchumi.

Miaka saba baadaye, ikaidhinishwa siasa huria na kumeya tena vyama vingi. Ndio kipindi katika jamii nako kukamea mijadala ama Ujamaa upo au umefikia ukomo.



Ndivyo zilivyokuwa nyendo za kilimo cha pamoja, katika harakati za kijamaa nchini. **PICHA: MAKTABA**

Nchi ikaendelea kutumikia Katiba ya Mwaka 1977 katika zama za muungao wa vyama TANU na ASP, kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambayo katika sehemu yake, inatamka kuendelea kutumikia Ujamaa.

Vilevile katika Sera ya Elimu nchini inagusa nafasi ya kuwapo Elimu ya Kujitegemea, inayotokana na itikadi ya Ujamaa, zao la Azimio la Arusha - 1967, ikichochea mijadala ya ama kutetea au kupinga maudhui hayo.

Hata hivyo, inapohojiwa maana ya Ujamaa hubaki swali gumu wengi wanaolijadili, wanashindwa kulijibu.

Hilo lilkajitokeza mwishoni mwa miaka ya 1990, pale Rais Benjamin Mkapa, alipounda tume chini ya Jaji Robert Kisanga kukusanya maoni ya wananchi kuhusu kuundwa katiba mpya.

Tume hiyo ilikutana na wanasheria jijini Dar es Salaam, katika ukumbi wa British, kupitia kivuli chao cha Chama cha Wanasheria Tanzania (TLS). Katika hoja walizopendekeza ni 'kuondolewa kipengele cha Ujamaa kwenye katiba iliyoko.

Pale walipotakiwa kufafanua sababu zao walikwama kutoa majibu yanayojitosheleza na hata lipotakiwa kutoa maana ya Ujamaa, likabaki swali gumu kwa wanasheria.

Alipotakiwa kusaidia kujibu Rais wao, Bob Makani, aliyewahi kuwa Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), pia muasisi wa chama - Chadema, naye akakwama, hata wajumbe wa tume kusita kusita kupokea hoja hiyo ya Ujamaa, wakiwataka wakasake maana, warejee nayo.

Kimsingi, ugumu wa swali hilo una mzizi mirefu, hata kuwa moja ya mambo yanayozaa utata kutafsiri ama Ujamaa upo au haupo, ikizingatiwa kuanzia mwanzoni mwa miaka 1990, kuna mengi kisera na kisheria yamebadilika kitaifa.

Hapo inagusa maeneo ya fedha na benki kuhalalishwa kisheria, pia elimu kuguswa na mabadiliko ya mitaala, mathalan kuondolewa somo Elimu ya Siasa na kuingizwa Uraia.

Tangu ya kufanyika mabadiliko hayo, wanazuoni hasa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), baadhi waliobobea katika sayansi ya siasa na sheria walijitokeza kulijadili kitaaluma.

Hapo katika nafasi kipekee majina kama mkongwe Profesa Samuel Mushi na waliofanana naye kitaaluma, maprofesa Mwesiga Baregu, Haroub Othman, Wamba dia Wamba (wote marehemu) na Dk. Ringo Tenga, walizama kwa kina kulijadili.

Nguzo mojawapo lililotumika katika kuongoza mijadala katika taaluma ya sayansi ya siasa, ulichorwa mstari mrefu wa kitaaluma wenye alama 100, unaogawanya kila upande alama 50 kutoka katikati, penye alama sifuri.

Mwanazuoni wa UDSM wakati huo, akiwa Msudani Kusini, Alfred Lokuji (sasa profesa) ana ufafanuzi wake kwa mfano wa mrengo kushoto (Ujamaa) ni: "Ukitoka katikati kwenda kushoto (kulia kwa msomaji), una maana unazidi kupata mchango wa moja kwa moja wa serikali kusaidia kuhudumia mtu (lakini ikitoza kodi zaidi)."

Pia, kinyume chake anataja ni mrengo wa kulia, serikali inatoza kodi kidogo, ikiacha nguvu za soko zifanye kazi na kwa kiasi kikubwa anayehudumiwa anajigharamia, serikali ikinufaika na kodi pekee na kuratibu nyendo za maisha.

Kwa ujumla wake, si rahisi sura hiyo kuchukua ama mrengo wa kushoto au kulia pekee, bali mrengo wa kushoto au kulia hutofautiana kwa asilimia nyingi.

Wanazuoni kama maprofesa Baregu, Othman na Mushi, walitofautisha Ujamaa katika sura tatu, zote zikiwa katika ujumbe "watu kuishi pamoja na kufanya kazi Pamoja, kwa faida ya pamoja."

Kutumia uwasilisho wa Profesa Othman, Ujamaa wa kwanza akautaja ni wa Kikomunisti, uliopatikana sana katika mataifa ya Mashariki, ikiwamo USSR, alikosoma yeye; ambako uendeshaji njia kuu za uchumi, pia maisha kijamii na kisheria yalisimamiwa na serikali.

Eneo la pili, kuna Ujamaa wa Kiafrika uliopatikana nchini kwa Rais Nyerere, aliyependa kutafsiri kwa kauli "watu wazima wanakusanyika kwa kina ya wote, wanakaa na kufanya maamuzi, kisha yanatekelezwa Pamoja, kwa faida ya wote."

Hapo akatumia mfano "ni kama katika jamii ya Kiafrika watu wazima wanaoheshimika wakakusanyika kwa niaba ya watu wao, kutafakari na kuamua mambo kwa niaba ya wote."

Mwisho, wasomi hao wakataja penye mfumo huria duniani kama nchi za Magharibi, kunakotoa haki sawa hasa kiuchumi, kwamba serikali inajiwekeza katika maslahi ya umma, ikiwamo kumiliki mashirika ya umma muhimu, mfano katika itikadi za vyama vya Democratic cha Marekani na wenzao Labour wa Uingereza.

Hata msingi wa kuzaliwa chama hicho cha Labour, inaanzia kuungana na jamii ya wafanyakazi Uingereza, ambao hawakuwa na chochote, nguvu kazi zao kutumikia ajira ilipofikiwa mapinduzi ya viwanda duniani.

### SURA YA MAGEUZI

Wakati kunafanyika mageuzi ya kisiasa na kuchumi kuanzia mwaka 1985, nchi ilifanya mabadiliko makubwa kutoka sura ya siasa na uchumi hodhi, kuelekea huria, mageuzi yaliyochukua hatua, pia taifa ikapitia changamoto kadhaa.

Mwanzo, ni kwamba Serikali Awamu ya Pili ilipokewa na magumu makuu matatu; ukosefu wa mafuta petroli mfumuko wa bei kufika zaidi ya asilimia 25; msuguano wa kisiasa kulazimisha kuingia vyama vingi, ulioanzia ulingo wa kimataifa.

Nne, kukawapo hitaji la nguvu kubwa ya kufanikisha kufikia mabadiliko kutoka mfumo hodhi hadi huria, vivyo hivyo unahusu dini, ambayo Rais Mwinyi alimaliza kipindi chake cha miaka 10 katika mustakabali huo.

Hapo hatosahaulika kubuni mengi ya maboresho katika mageuzi ya elimu ya juu, kutanua nafasi, pia aina za taaluma, ambayo kimsingi ndio chimbuko la kuanzishwa Chuo Kikuu Huria (OUT) nchini.

Katika awamu ya tatu ya uongozi Rais Mkapa, akatangaza kuzama zaidi katika mrengo wa kulia, serikali kubakia kuwa mratibu mkuu wa uchumi, jamii na siasa, utendaji biashara na uchumi zaidi kuwa wa umma.

Wakati ikiendeleza maboresho ya kiutendaji kiuchumi, Tume ya Rais ya Kubinafsisha Mashirika ya Umma (PSRC) ikiendeleza majukumu yake, ikabainika baadaye katika baadhi ya maeneo haikufanikishwa.

Msingi wake, PSRC ilibinafsisha kwa uwiano unaokaribiwa kwa baadhi ya taasisi yaliyosuasua, kati ya serikali na vyombo binafsi; pia yenye hali mbaya hisa kubwa au zote ziliuziwa wahitaji binafsi.

Kulikuwapo asasi ambazo hisa zake wakauziwa watumishi wamiliki, mfano Kiwanda cha Uchapaji cha Taifa (KIUTA) na kiwanda cha maziwa mkoani Tanga. Mfuko unajulikana kama MEBO (Management by Ownership).

Aina ya mwisho, ni katika ubinafsishaji wa kukodisha kampuni kwa muda maalum, kisha serikali inarudishiwa mali yake, iliyofanyika kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC) kukodishiwa mteja wa India, hata hivyo haikufanikisha malengo na mkataba wake ukavunjwa ndani ya muda mfupi.

Kwa ujumla, uzoefu wa utekelezaji uliofanyika katika awamu ya tatu, ni baadhi ya kasoro katika ubinafsishaji wa mashirika ya umma, hayakukidhi matakwa na kampuni zilizobinafsishwa zikatoweka.

Hadi inamaliza muda wake, serikali ya awamu ya tatu ikawarejea wananchi katika tafsiri ile ya Msomi Dk. Lokuji "serikali haiwezi kuwaacha watu wake kuwa wahanga wa nguvu zas soko", pale ilipoamua kuirfanya mapitio yake, ikafanya ubunifu kuboresha elimu, ikianzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na kituo kama hicho kwa sekondari kiitwacho MMES.

Katika lugha rahisi ikarejesha mrengo wa kushoto amboa ni utashi wa Ujamaa.

### AWAMU YA NNE

Serikali ya Awamu ya Nne, iliingia madarakani na mada kuu tatu; mosi kuendeleza zao la MMES, shule za kata zilizobuniwa na mtangulizi wake, Benjamin Mkapa.

Mrithi Jakaya Kikwete, akaboresha elimu kwa operesheni maalum kuimarisha mahitaji taaluam na majengo ya Sekondari Kata, kwa opreresheni maalum iliyosimamiwa na Waziri Mkuu, Edward Lowassa.

Pia, Rais Kikwete akaekeleza vyuo vikuu vyote nchini kuwa na vitivo vya ualimu, akiwa na upendeleo kwa wanaosomea kupata mikopo, hatua kama hiyo kwa kwa vyuo vikuu vipya na hatya Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine.

Mikakati hiyo ikaendana na kuanzishwa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), uliokuwa ubunifu wake Kikwete, sambamba na kipaumbele cha uwekezaji mkubwa katika barabara na madaraja nchini.

Hiyo ni hata mikoa kama Rukwa, Mtwara, wilaya Tunduru, mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kigoma ifunguke kibarabara, kukirejeswa baadhi ya mashirika ya umma.


Akahitimisha muda wake, akibuni wazo la kuanzishwa reli ya kisasa, SGR, mradi ambao hakutekeleza kutokana na mzigo wa miradi mitatu, MMAM, Barabara na MMES, iliyogharimu taifa, tena kwa mzigo wa mikopo.

Kwa ujumla wake, tafsiri ya ujamaa katika mfumo huria imechukua nafasi, kama anavyotafsiri mwanazuoni Dk. Lokuji kwamba kwenye Ujamaa "serikali inadumu kuwa sehemu ya jamii na daima haiwezi kuwaacha watu wake wateseke na shinikizo la soko huria."

***• Soma zaidi Awamu ya Sita na Uchumi Ujamaa. Uk 14.***

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Kwa utangazaji huu hakika tunavuna mabua






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

ZAMANI wakati kuna vituo vichache tena vya kuhesabika vya redio, achilia mbali luninga ambayo haikuwa akilini mwetu, tulihimizwa sana utulivu wakati wazee wetu wakisikiliza taarifa za habari au mijadala ya kuelimisha umma.

Lilikuwa kosa la jinai kifamilia, baba au mama anasikiliza redio halafu wewe unapiga kelele, au kuleta mchezo unaosababisha kuondoa utulivu wa masikio ya wasikilizaji hao.

Bila shaka kama mjeledi au mkwaju vilikuwa mbali, hukukosa kofi, kibao au kwenzi la nguvu kutoka kwa wakubwa hao ukaugulie, ili kurejesha utulivu na taarifa ya habari isikike vizuri na hasa siku ambayo Mwalimu Nyerere alizungumza.

Lakini kulikuwa na vipindi kama Chakula Bora na hata cha Michezo, ambako kila mwenye timu yake, alitaka kujua imefanya nini au kulitokea nini katika mechi zipi siku hiyo.

Vipindi kama Majira, Watoto Wetu na Utabiri wa Hali ya Hewa vilipendwa sana, kwani vilijulisha matukio ya siku, pia kunyesha au kutonyesha mvua na hata radi na kuziepuka pamoja na kuelimisha watoto.

Nakumbuka kipindi pekee kilichokuwa na mbwembwe ni cha Klabu Raha Leo, pia Misakato, ambayo bendi za muziki wa dansi zilikwenda studio kurekodi na kupiga muziki mubashara, pia nyimbo mpya zilizosikika mtawalia.

Watangazaji wa vipindi hivyo hususan vya taarifa, walitulia na hakuna aliyesikika akikohoa au kupiga chafya, achilia mbali kupasuka kicheko cha kuvunja mbavu, isipokuwa kipindi cha Mahoka!

Ingawa hakukuwa na wasomi wengi kama sasa, lakini watangazaji walitumia Kiswahili fasaha na usingesikia mahali wanachanganya na kilugha chao au hata lugha ya kigeni hususan Kiingereza.

Na kama walilazimika kutumia Kiingereza, ilikuwa ni katika idhaa ya Kiingereza, ambayo kila kitu kilikwenda kwa lugha hiyo, bila kuingiza Kiswahili au lahaja yoyote.

Tunaambiwa studio kulikuwa na msimamizi wa kipindi, ambaye alihakikisha kila kitu kinakwenda kilivyopangwa, bila mtangazaji kuchanganya mbwembwe.

Leo hii, tuna vituo kibao vya redio mpaka vijijini, huku vikizidiana kwa ukubwa unaoendana na ukwasi wa wamiliki, ambao sasa vimekuwa ni miradi ya ujasriamali.

Ndivyo pia vipindi vinavyopangwa kijasiriamali.

Tofauti na awali, hivi sasa msikilizaji ndiye anakimbia kelele zinazopigwa na watangazaji, wakishindana kupaza sauti, ili kila mmoja asikike kuwa ndiye gwiji katika mada kuliko mwenzake, wakikatishana hapa na pale.

Aliyeanzisha kituo leo hatofautiani na aliyeanzisha jana, kwa sababu ya kuigana maudhui. Ukianzisha cha michezo, nami nakuja na cha michezo, sawa tu na mama lishe mtaani, akiuza vitumbua na mwenzake anaiga.

Kinachonisikitisha sasa, ni utiriri wa vituo ambavyo vimeanzisha vipindi vya michezo, vinavyotawaliwa na wachambuzi, baadhi yao wakijifanya kujua michezo kuliko hata wachezaji na makocha wao.

Nongwa zaidi ni pale wanapotumia zaidi Kiingereza katika vipindi vya Kiswahili, ambavyo hata hivyo vina majina ya Kiingereza! Ni mshangao mtupu! Unajiuliza wanamtangazia nani nchini? Mwingereza au Mswahili?

Aachiwe mwalimu wa kigeni watimu atiririke Umombo sasa, nani wa kufasiri? Thubutu! Utaambiwa tu kama mlivyomsikia kocha...!

Juzi asubuhi ikabidi niamke kitandani, nikakaa nisikilize kipindi fulani hivi cha watangazaji wanaojifanya mahiri, wakiwa wamemwalika mbunifu studio kuzungumzia ubunifu wake.

Nikamsikia mmoja akisema, nchini wabunifu hawatambuliwi wala kujaliwa kama wa kigeni, akasema ukitaka ubunifu wako utambuiliwe labda basi ufuatane na Mzungu hata kama ni kichaa, ili mradi awe karibu na wewe.

Kwamba Mzungu anapewa kipaumbele kuwa ndiye hasa anaweza kubuni jambo likakubaliwa katika jamii ya Kitanzania. Wakati nashangaa hiyo, nikidhani mtangazaji mpenzi anasema hivyo kwa dhati, nikamsikia papo hapo anachanganya Kiswahili na Kiingereza katika kauli zake.

Nikamwona na yeye kama hajui akisemacho, kwani anampiga vita Mzungu, huku naye akishindwa kujiamini, kwamba hawezi kuzungumza Kiswahili muda wote, bila kuchaganya, kwani hataonekana anajua kazi anayofanya!

Msomaji wangu, ukisikiliza vipindi vya michezo vyenye wachambuzi, kama hujui Kiingereza basi acha tu kuhangaika, kwani hutaambulia kitu ingawa hata hao Watangazaji wanaojinasibu kukijua, hawakijui ila wanachomekea maneno ambayo pia si yenyewe, ila yanafanana na Kiingereza.

Zamani, watangazaji wetu, ingawa nao walikuwa vijana, lakini hawakutangaza kujitafutia kiki kama tuwasikiao leo, wakipiga kelele na kukatizana kauli na hata wakiwa na wageni watawakatiza hata kabla hawajamaliza kujieleza.

Hali hiyo, si tu inatuchanganya wapenzi wasikilizaji wao, bali inatuchosha masikio na kutamani hata kukaa vijiweni kusikiliza soga za soka za huko, badala ya watangazaji ambao huingia studio bila kujiandaa na badala yake kukosoa kishabiki bila kuzingatia ukweli. Jirekebisheni bhana. Oriti uru!

MIAKA 64 YA UHURU...

# Zama za Dk. Samia na Ujamaa katika uchumi – siasa zinavyosafiri nchini

***KATIKA** uchambuzi wa ukurasa wa 12, ulikuwa na mustakabali mpana wa tafsiri na nafasi ya Ujamaa, ndani ya mabadiliko ya kihistoria, Tanzania inapitia. Je swali linabaki, katika uongozi wa Awamu ya Sita, nini nafasi ya Ujamaa? Pata ufafanuzi wa mwandishi **PETER ORWA.***

WAKATI mikakati ya kiuchumi ikiendelea nchini, unapoingizwa muktadha wa ama mwenendo wa kiserikali unaendeshwa na siasa za Ujamaa, au sivyo ni zao lenye jibu kwa 'hoja kwa vielelezo.'

Kikubwa cha uzoefu ni katika Awamu Tatu za uongozi kiserikali nchini, hasa kuanzia zama za uongozi wa marais Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete na John Magufuli, kuna nyendo za Kijamaa zimetumika, ndani ya mustakabli wa mfumo huria.

Mosi, uhalisia unaanzia katika Katiba ya Nchi (inayojadiliwa) inagusa kutambua matumizi ya nyendo hizo, pia Sera ya Elimu iliyopo ya mwaka 2014, inatumia 'Elimu ya Kujitegemea' ambayo ni zao la Azimio la Arusha, ikiwa na maana ya Ujamaa katika tafsiri yake "Njia Pekee ya Kujenga Jamii ya Watu Walio Sawa na Huru."

Hadi sasa uongozi wa Rais Dk. Samia, unadumu nayo Elimu ya Kujitegemea, ambayo inabeba maudhui makuu kadhaa yaliyobuniwa na Rais na Mwenyekiti wa chama tawala - TANU mwaka 1967.

Mosi, ilitaka elimu ya kitanzania kurejea maudhui ya maisha ya utanzania; kila anayepata elimu hiyo akanufaishe umma wake; kila ngazi ya elimu ijitosheleze na kuweza kutumika.

Hapo ikamaanisha ngazi anayohitimu shule ya kitanzania, iweze kutumika kwa ufanisi na si mhusika kuhesabika hajafaulu na ndio maana walioshindwa mitihani darasa la saba, walitafsiriwa 'hawajaendelea' na siyo 'kufeli', huku walioshinda mtihani 'wamechaguliwa kujiunga sekondari.'

Bado ambao hawakuchaguliwa walitarajiwa elimu yao kuwafaa katika shughuli zao kimaisha mfano shambani. Hiyo ni sababu mojawapo katika shule za sekondari kuanzishwa mikondo; Biashara, Ufundi, na Sayansi.

Wakati katika mfumo wa kiuchumi ukiwa hivyo, serikali inazama zaidi katika mrengo wa kulia kuzalisha, serikali ikibaki mratibu mkuu na kukaribisha uwekezaji, mathalan kasi inayoendelea kukaribisha viwanda vya mbolea nchini.

Pia, hatua kama hiyo ndio iko katika kukodisha uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Hata hivyo, serikali katika upande wa pili wa shilingi, ikawajibika moja kwa moja katika kuziba mapengo ya shida za kijamii zinazojitokeza, hasa pale nyenzo binafsi zinapokwama.

Hapo ni katika maeneo kama viwanda vya sukari, vilivyo chini ya mifuko ya uwekezaji kukabili uhaba wa sukari kitaifa, vivyo hivyo kwa kuanzisha kiwanda cha viuatilifu.

Ni dhana inayoenda mbali katika mustakabali wa elimu, pale yalipoonekana mapengo katika fursa za kielimu na kiafya, serikali imeingilia moja kwa moja.

Kuanzia na safari ya kihistoria, pengo la elimu ya sekondari kuanza kuzibwa kiserikali kupitia kubuniwa sekondari za kata katika awamu ya tatu ya uongozi, ikaenda mbali kuboreshwa kimahitaji katika awamu ya nne.

Inapotajwa, uongozi wa awamu ya tano Rais Dk. Samia akiwa Makamu wa Rais, ulibaini ada ya Sh. 20,000 kwa sekondari ulikwamisha baadhi wazazi kupeleka watoto shule, hata ikafutwa rasmi hadi kidato cha nne.

Lakini hilo likaonekana kuwa ni tatizo bado na ilipongia serikali ya awamu ya sita, ikafuta hadi kidato cha sita, kwa ujumla wake ukaongeza ujio wa wanafunzi wapya maradufu, sambamba na shinikizo la kisheria, hata wakamiminika wanafunzi wengi wakiwamo kutoka jamii za wafugaji.

Hatua kama hiyo, ikafanyika hata katika ngazi ya elimu ya juu, iwe haki ya kila mtoto wa Kitanzania, hasa pale katika Awamu ya Sita ya uongozi wa nchi, Rais Dk. Samia akatangaza kupanuliwa fursa na haki za wanafunzi wa elimu ya juu kupata mikopo ya elimu, si ngazi ya vyuo vikuu pekee, bali hata wa chini yao wanaosomea diploma.



Mjumuiko wa kinamama waliokutana na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani) jijini Dodoma, 2021. **PICHA: MTANDAO**

Pia, Rais katika awamu iliyoko sasa, akawaandalia wahitimu urahisi kwamba, mikopo hiyo sasa itarejeshwa bila ya riba na kuwa haki ya kila mwanafunzi na si makundi fulani pekee.

Hapo ikirejewa tafsiri hiyo kisiasa, ni utekelezaji wa nguzo ya kijamaa ndani ya mfumo wa uchumi huria, kama ambao unatumiwa na vyama vya Labour Uingereza na Democrat, Marekani.

Kuna marejeo hapo ya mgombea Barack Obama wa Marekani, alitumia shida ya watu wa chini katika afya, kuanzisha bima ya afya rahisi kwa wengi na ikamvusha kisiasa

### NAFASI JINSIA

Eneo lingine la tafsiri ya Ujamaa huria, ni pale Rais Dk. Samia akawekeza jinsia yake kunadi hali za wanawake wanaokwazwa katika mengi kisiasa.

Kurejea katika fursa za elimu ya juu, ikiwamo kuwa na mifuko ya kusomesha mabinti hata inawawezesha kitaaluma, ambayo zao lake inawang'arisha mbele kimaisha. Pia, kwa kutumia Mpango wa Maendeleo ya Msingi (MMAM) ameboresha huduma za vituo kwa ujenzi na upanuzi wa vyuo vingi sana vya afya kitaifa, ambayo katika hali halisi umma, ndio unamudu kuliko binafsi.

Sura hiyo ndio kuna kundi kubwa la kinamama wanaopewa fursa za kiutendaji katika uongozi, ikionekana wazi sasa kuanzia ngazi ya chini hadi Baraza la Mawaziri.

Mtazamo wa wote, unarejesha katika majumuisho ya nadharia za kijamaa, pale kunapokuwapo mapengo ya kijamii, hasa katika kundi la waliokosa kufanyiwa upendeleo wa kisiasa wanufaike.

## Kikundi kinamama wamechanga Sh.500 kila mmoja kwa siku, wanunua basi

**INATOKA UK.11**

Mkurugenzi Koti, ambaye pia ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, akawataka wadau kuwaunga mkono kwa lengo lao kuzifikia shule zote nchini.

Anasema, wameanzia katika shule hiyo kwa sababu walimu walikubali kupunguza fedha katika mishahara yao ya miezi mitatu, kuchangia vifaa na kuwanunulia wanafunzi wenye uhitaji.

Anasema. kwake limekuwa jambo kubwa na faraja kuona walimu wanaunga na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji, jambo ambalo miaka ya nyuma halikufanyika.

"Hamasa kubwa imetokana na viongozi niliowakuta na mimi ninapenda maendeleo, lengo letu mwakani tutafanya kwa kata nzima ili ikiwezekana shule zote zipate alama 'A' katika mitihani yao.

"Hii ni kwa sababu serikali inatoa elimu bure mchango wetu ni kusaidia mambo madogo madogo kwa miaka mitatu mfululuzo nimeikuta Ilala inaongoza ndio mana nikaamua kuja na huu mapango ili wanafunzi wabaki na jukumu la kusoma pekee.

"Baada ya kukusanya kwa walimu tukaja kwa viongozi wakata, baadhi ya wazazi pia walishiriki na vifaa vilivyopatikana vimetosha kwa wahitaji na yaliyobaki tutayahifadhi, kwaajili ya kusaidia shule nyingine.

"Sisi kama mfuko rasmi, vifaa hivyo, tumevielekeza kwa wenye changamoto tunataka kuonyesha upendo tupo tayari kushirikiana na viongozi pamoja na Rais Samia kufanikisha mambo madogo madogo.

### DIWANI ILALA

Diwani wa Kata ya Ilala Sadi Kimji, alimpongeza Koti, kwa juhudi zake kuboresha elimu, akisisitiza shule hiyo imekuwa mfano wa kuigwa kutokana na matukio yao yanayoashiria kufunga mkono juhudi za serikali katika utoaji wa elimu.

"Tunawapongeza na kuwashukuru sana na sisi kama viongozi... Ng'ara Foundation tutaipa kipaumbele kuhakikisha inafikia malengo haya ya kuendelea kusaidia wanafunzi wenye maisha magumu ikiwamo yatima" anasema, huku akishangiliwa na wazazi wa watoto waliokuwapo katika tukio hilo

Akihitimisha, Juliana anasema, wameanzia shule hiyo, kwa sababu hata walimu wake walionyesha nia kuchangia.

"Hii imetokana na ushirikiano mzuri kati ya Mwalimu Mkuu Andrew Koti, na walimu wake kwa kuweka mazingira rafiki," anahitimisha.



# Malimbikizo mishahara watumishi wa umma kujadiliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKUU wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu serikalini wanatarajia kujadili changamoto ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu kikao kazi hicho Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Xavier Daudi, alisema kitakafanyika kwa siku tatu jijini hapa kuanzia Desemba 17 hadi 19, mwaka huu.

Daudi , alisema washiriki wa kikao kutoka wizara, taasisi za umma na serikali za mitaa, pia watajadili na kupeana maeneo ya vipaumbele vya serikali na aina ya watumishi wanaotarajiwa kuajiriwa kwa mwaka husika.

Alisema washiriki hao pia watabadilishana mawazo na kupeana maelekezo kuhusu vipaumbele vya serikali kwenye ajira, maandalizi ya ikama na bajeti ya mishahara.

Daudi, alisema vilevile watakutana kujadili mambo yanayojitokeza kwenye utekelezaji wa majukumu yao ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Malengo hasa ya kikao kazi hiki ni kubadilishana uzoefu, tunajua utumishi wa umma ni mpana na nchi yetu ni kubwa, wale wanaofanya vizuri wanaongea na wenzao na wanabadilishana zile changamoto ili tuwahudumie Watanzania vizuri, tunakumbushana mambo ya msingi maana tunajua sekta au wizara na taasisi zimekuwa na mabadiliko mengi hasa kwenye mifumo," alisema.

**"Tumeona yana changamoto na tunaweza kuwashirikisha na kutengeneza njia bora ya kutatua kwa watumishi wetu waliopo taasisi za serikali."**

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Ibrahim Mahumu, alitaja maeneo mengine ambayo watajadili kuwa ni maandalizi ya ikama ya bajeti ya mishahara na usimamizi wa rasilimaliwatu.

"Kwenye usimamizi wa rasilimaliwatu kuna eneo la usimamizi wa mishahara na baadhi ya changamoto zinakabili eneo hilo, tunaweza kuongea na wenzetu hasa kwenye eneo la uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu kushughulikia majukumu na haki za watumishi, " alisema na kuongeza kuwa:

"Tumeona yana changamoto na tunaweza kuwashirikisha na kutengeneza njia bora ya kutatua kwa watumishi wetu walioko taasisi za serikali."

Kadhalika, alisema eneo la maandalizi kama na bajeti ya mishahara litajadiliwa kutokana na kuwa na changamoto na ofisi hiyo ndio yenye jukumu la kusimamia maandalizi hayo kwa watumishi hao wa umma.

"Tunaelekea mwisho wa mwaka huwa kuna maandalizi ya ikama na bajeti ya mishahara, kwa hiyo kuna mambo mengi ya kuwekana sawa ili wanapoanza kubainisha mahitaji ya watumishi wanaopaswa kuajiriwa ni vizuri kupeana maeneo ya vipaumbele vya serikali ili kujua mahitaji yao na aina ya watumishi wanaopaswa kuajiriwa kwa mwaka husika," alisema.

Mkurugenzi wa Utawala wa Utumishi wa Umma, Felister Shuli, alisema wakuu hao watajengewa uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi na kusimamia rasilimaliwatu kwenye maeneo yao.



Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Shila Mwashiuya (kulia), akikabidhi mashine ya kufuma sweta kwa mlemavu wa miguu, Rehema Juma iliyotolewa na Shirika la Sightsavers kupitia mradi wa uwezeshaji kiuchumi kwa watu wenye ulemavu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama na Manispaa ya Singida, juzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Marufuku kukata miti vichaka vya Itigi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MKUU wa Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, Dk. Vicent Mashinji amepiga marufuku ukataji miti ili kulinda uoto wa asili wa vichaka vya Itigi na kuongeza mapato ya serikali.

Dk. Mashinji alitoa amri hiyo juzi katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Itigi iliyopo katika wilaya hiyo cha robo ya pili.

Alifafanua kuwa ametoa amri hiyo ili kulinda uoto huo kwa kuwa una uwezo mkubwa wa kuondoa kaboni kwenye hewa na kutumika kama chanzo cha mapato ya halmashauri hiyo.

Alikitaka kila kijiji kiweke akiba ya misitu na kuhifadhi vichaka hivyo kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hussein Simba, alisema kwa robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha 2024/2025 wamekusanya mapato kwa asilimia 50 kutokana na ushirikiano mzuri baina ya wataalamu na madiwani

Simba alisisitiza usimamizi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo ya halmashauri hiyoikamilike kwa wakati na kuleta tija kwa jamii

Katibu Tawala Msaidizi wa Viwanda,Biashara na Uwekezaji Mkoa wa Singida, Donatila Vedast, aliitaka halmashauri hiyo kutenga maeneo na kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji hasa katika kilimo ili kuharakisha maendeleo ya halmashauri na wananchi.

Katibu Tawala Wilaya ya Manyoni, Leila Sawe alisisitiza ukamilishaji wa miradi viporo na kuanza kutumika.

Kaimu Mwenyekiuti wa Halmashauri hiyo, Jonathan Dule, ameipongeza halmashauri kwa kuvunja rekodi ya ukusanyaji wa mapato kwa katika kipindi hicho.

## Wajasiriamali waongezewa mikopo

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB) inatarajia kuongeza kiwango cha kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati nchini kwa lengo la kuboresha biashara na kuwaepusha na mikopo umiza.

Mwenyekiti wa Baraza la wafanyakazi la benki hiyo, Daniel Mroto alitangaza mpango huo jana jijini hapa katika mkutano wa baraza hilo kujadili mikakati ya kuboresha huduma za benki hiyo na kufanya tathmini za utendaji.

Mroto, alisema hadi kufikia Novemba mwaka huu, wametoa mikopo kwa wajasiriamali ya Sh. bilion 300 na kwamba kufikia mwakani wanatarajia kuongeza kiasi hicho.

Alisema wameweka mifumo mizuri ya utoaji mikopo kwa wajasiriamali hao na kutoa wito kujitokeza kuchangamkia fursa hiyo.

"Dhamira ni kuona jamii inanufaika na mikopo inayotolewa na taasisi za serikali, wajasiriamali mnapaswa kuchangamkia fursa za mikopo," alisema Mroto.

Katibu wa baraza hilo, Colimba Tawa, alisema kazi yao ni kuishauri menejimenti ya benki hiyo kufanya kazi kwa ufanisi na kufikia malengo yao kwa mwaka ujao.

Tawa, alisema moja ya mikakati waliojiwekea ni kuhakikisha wanaboresha huduma za jamii na kuhamasisha wananchi kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali ikiwemo benki hiyo.

Alisema wao kama baraza la TCB wataendelea kutoa ushirikiano wa utendaji kazi na benki hiyo ili kuhakikisha wanafikia malengo ya kimkakati ambayo wamejiwekea kwa mwaka huu na ujao kwenye utendaji wao.

"Baraza hili litakuwa mstari wa mbele kuishari TCB kuhakikisha malengo yao yanafanikiwa,ikiwemo utoaji wa huduma kwa jamii inayotuzunguka,"alisema Tawa.

Hata hivyo aliwasisitiza jamii pamoja na watumishi wa umma kuchangamkia fursa zinatolewa na benki hiyo kwa ajili ya kujiinua kiuchumi ikiwemo kufanya maendeleo wao na familia zao.



# TBS waagizwa kudhibiti bidhaa za magendo

**Na Mwandishi Wetu**

MENEJIMENTI ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imeagizwa kuweka mikakati ya kudhibiti bidhaa zinazoingia nchini kwa njia za panya kwa lengo la kukwepa kulipa ushuru na kuepuka madhara kwa watumiaji kwa kukosa ubora.

Agizo hilo lilitolewa jana mjini hapa wakati wa ziara ya Bodi ya Wakurugenzi ya TBS na Mwenyekiti wake, Profesa Othman Chande ya kutembelea ofisi hizo zilizopo mipaka ya Tunduma Wilaya ya Momba Mkoa wa Songwe na Kasumulu wilayani Kyela (Mbeya) ili kujionea shughuli zinazofanywa.

Profesa Chande, alisema TBS inatakiwa kuweka mitego ya kukamata bidhaa zinazoingizwa kinyemela kwa kufanya ukaguzi na kuendelea kutoa elimu ya madhara ya kutumia bidhaa ambazo hazijathibitishwa ubora na shirika hilo.

Alisema dhumuni la ziara hiyo ni kubaini changamoto zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi .

Aliielekeza menejimenti ya shirika hilo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na kuwezesha biashara.

**“Bodi imeielekeza menejimenti ya TBS kuja na mikakati ya bidhaa zinazoingia kupitia njia za panya, tunataka bidhaa zote zipitie njia halali kwa sababu njia za panya zinaingiza bidhaa hafifu,” alisema.**

Chande, alisema pamoja na TBS kuwa na wakaguzi wanaoshirikiana na mamlaka nyingine za udhibiti kwenye njia rasmi za kuingizia bidhaa nchini mipakani, viwanja vya ndege na bandarini, bado kuna changamoto ya bidhaa kuingizwa kwa njia za panya.

“Bodi imeielekeza menejimenti ya TBS kuja na mikakati ya bidhaa zinazoingia kupitia njia za panya, tunataka bidhaa zote zipitie njia halali kwa sababu njia za panya zinaingiza bidhaa hafifu,” alisema. Alisema bodi hiyo imeagiza menejimenti hiyo kuhakikisha bidhaa zilizokaguliwa kutoka nje na zinazozalishwa nchini kuwa na alama maalum kumtambulisha mlaji wa mwisho wa matumizi ya bidhaa na kumuepusha na madhara ya kiafya

Agizo hilo limetolewa kufuatia Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk Ashura Katunzi kueleza kuwa bidhaa ambazo hazijakaguliwa na shirika hilo vikiwemo vipodozi vilivyopigwa marufuku, zimeendelea kuwepo kwenye soko la ndani kutokana na baadhi ya wafanyabiashara kutumia njia za panya kuingiza nchini.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Heri James akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo maalum ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Usalama za Mkoa wa Iringa, yanayoratibiwa na Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, wilayani humo, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mkandarasi aamriwa kujenga miradi ya maji usiku, mchana

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

NAIBU Waziri wa Maji, Kundo Mathew amesema hajaridhishwa na kusuasua kwa ujenzi wa miradi mitatu ya maji ya miji 28 na kutoa miezi miwili kwa mkandarasi kujenga usiku na mchana ili kukamilisha na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Mathew, alitoa amri hiyo juzi baada ya kukagua miradi hiyo inayotekelezwa katika halmashauri za miji ya Njombe, Makambako na Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe na kubaini kuwa haijakamilika kwa kiwango kikubwa.

Alisema kasi ya ujenzi wa miradi hiyo yenye thamani ya Shilingi bilioni 205.93 hairidhishi kutokana na kushindwa kuendana na kasi na mahitaji ya wananchi na mkataba baina ya Serikali na mkandarasi huyo.

“Naona tupo nyuma ya wakati tukimaanisha shughuli zote kulingana na ratiba ya kazi ambazo zilikuwa zimepangwa zote ziko nyuma ya zaidi ya siku 90 na kuna nyingine ni nyuma ya siku 100 maana yake tunachechemea,” alisema Mathew.

Alisema wakandarasi wanapaswa kuongeza nguvu kwa kuweka wafanyakazi wengi kwa sababu waliopo ni wachache hali inayosababisha mradi huo kusuasua.

“Muda ambao tumeupoteza tunaweza kuufidia kwa kuongeza wafanyakazi na saa, maana yake badala ya kufanya tisa wakafanya usiku na mchana,” alisema Mathew.

Alisema miradi hiyo ni ya kimkakati na kwamba serikali inataka kuhakikisha Mkoa wa Njombe unaongeza zao la upatikanaji wa maji safi na salama.

“Hii miradi mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kweli amewapendelea sana wananchi wa Njombe na nina hakika tutahakikisha miradi hii inasimamiwa kwa weledi na kukamilika kwa wakati kwa kuangalia thamani ya fedha,” alisema Naibu Waziri huyo.

Awali, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Njombe (NJUWASA), Robert Lupoja, alisema mradi huo kwa Halmashauri ya Mji wa Njombe wenye thamani ya Shilingi bilioni 40 ujenzi wake umefikia asilimia 13. Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Zakaria Mwansasu, alisema matumaini ya wananchi ya mradi huo ni makubwa, hivyo kasi ya ujenzi inapaswa kuongezeka ili wanufaike na maji safi na salama.

Baadhi ya wananchi mjini Njombe, akiwemo Aneth Odocha, alisema wanatamani kuona mradi huo unakamilika kwa wakati na kuwaondolea adha ya kutafuta maji kipindi cha kiangazi.

# Jamii yanyoosheana kidole walemavu kufungiwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

IMEELEZWA kuwa jamii kuogopa kutoa ushahidi kwa vyombo vya ulinzi na usalama wa matukio ya ukatili nchini kunachangia watoto wenye ulemavu kufungiwa majumbani na kukosa haki na elimu.

Hayo yalisemwa juzi na wakazi wa Mtaa wa Idofi katika kilele cha Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yaliyofanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Idofi.

Walisema wengi wao wanashindwa kuripoti matukio hayo kutokana na kuogopa lawama kwa familia yenye watoto wenye ulemavu.

Mmoja wa wakazi hao, Jackson Mchelu, alisema kuna watu wanashuhudia watoto wenye mahitaji maalumu wakifungiwa ndani na kuogopa kutoa taarifa kwa sababu ya kukwepa lawama.

“Mtu kama huyo anachohitaji kupata ni elimu kwa sababu hizo siku 16 bado ni chache, ikiwezekana ziongezwe ili elimu hii isambae na watoto waokolewe dhidi ya matendo haya,” alisema Mchelu.

Alecia Chungu, alishauri elimu ya ukatili watoto na wanawake itolewe wakati wote huku kutokomeza ubakaji, ulawiti, vipigo na wanandoa kutengana na kukiripotiwa mara kwa mara.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Njombe, Kassim Ephrem, aliitaka jamii kukemea vitendo vya rushwa kwani ni miongoni mwa sababu zinazochangia matukio ya ukatili wa kijinsia.

Awali Mkuu wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Kipolisi Makambako, Omary Diwani, alisema licha ya elimu ya ukatili kutolewa kwenye makundi mbalimbali, wamekutana na waganga wa tiba asili ili kukabiliana na matukio hayo yanayohusishwa na imani za kishirikina.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga aliwataka wananchi kuachana na mila potofu kwa kuwa zinachangia matukio ya ukatili kwa watoto.

Jeshi kwa kushirikiana na Idara ya Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Mji wa Makambako iliandaa maadhimisho hayo na kutoa msaada kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wa shule hiyo.



# CCM yajivunia Wazazi kuendelea kushika dola

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Mapinduzi (CCM) kimesema kinatambua na kuthamini kazi inayofanywa na jumuiya ya wazazi kukiimarisha na kuendelea kushika dola na kuwaongoza wananchi.

Kauli hiyo imetolewa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla katika hafla ya kukabidhi vifaa vilivyotolewa na Mbunge wa Wazazi, Najma Giga kwa Mkoa wa Mjini Kichama visiwani hapa.

Abdulla, ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, alisema vifaa hiyo vitaleta matokeo chanya kwa kila anayestahili kusajiliwa na kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga kura anapatiwa haki ya kuchagua viongozi katika uchaguzi mkuu ujao mwakani.

Hemed aliihakikishia jumuiya hiyo kuwa ataendelea kushirikiana nayo kufanya kazi za chama hicho na kupambana kiendelee kushinda kwa kishindo katika uchaguzi huo na nyingine zijazo nchini.

Alitamba kuwa CCM itaendelea kushika dola kutokana na sera zake na miradi ya maendeleo kutekelezeka kupitia ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025.

Makamu Mwenyekiti wa Wazazi Zanzibar, Dogo Iddi Mabruk, alisema jumuiya hiyo imeongeza kwa uandikishaji wanachama wapya wa CCM kwa mfumo wa kielektroniki na nguvu kukipatia ushindi katika uchaguzi huo mkuu utakaovishirikisha vyama vingi vya siasa nchini.

**Makamu Mwenyekiti wa Wazazi Zanzibar, Dogo Iddi Mabruk, alisema jumuiya hiyo imeongoza kwa uandikishaji wanachama wapya wa CCM kwa mfumo wa kielektron-**


Dogo alikitaka chama hicho kuiongezea nafasi za ubunge na uwakilishi jumuiya hiyo kutokana na kazi kubwa inayofanya ya kukiimarisha na kukipatia ushindi kwa kuwashawishi wananchi kukichagua.

Mbunge wa Viti Maalum wa Wazazi Mkoa wa Mjini, Najma Murtaza Giga, alisema lengo la kutoa vifaa hivyo ni kuboresha utendaji kazi katika jumuiya hiyo.

Najma, aliwasisitiza viongozi wa jumuiya hiyo kufanya kazi kwa weledi na umakini.

Aliwataka wanachama kushirikiana na jumuiya za chama hicho na kuacha makundi, majungu, kuunganisha nguvu na kuhakikisha wapata ushindi wa kishindo mwakani.

Alimtaka Abdulla kuwasaidia kupata sera ya malezi ya Mtoto Zanzibar ya kutoa miongozo ya malezi mema na yenye maadili ili kuwa na kizazi bora kitakachokitumikia Taifa kwa uzalendo.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Community Forests Pemba, Mbarouk Mussa Omar (kulia), akikabidhi kifaa cha umeme wa jua 'solar' kwa Mkulima Eshe Abdallah, wakati wa ugawaji wa vifaa vya kusambazia maji kwa wakulima wa kilimo mseto katika Kisiwa cha Uzi, Mkoa wa Kusini Unguja, juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi azungumzia matibabu nje ya nchi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya kupeleka wagonjwa wanaoambatana na ndugu zao kwenda nje ya nchi kupata matibabu.

Dk Mwinyi alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na madaktari wa Hospitali ya MIOT Chinnai ya India Ikulu Zanzibar.

Aliwapongeza madaktari hao ambao waliongozana na mwenyeji wao, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui na watendaji wakuu wa wizara kwa ajili mazungumzo hayo. Mwinyi alisema madkati hao wanastahilo pongezi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwahudumia Wazanzibari hasa wa magonjwa wa moyo, saratani na kiharusi.

Vilevile alipongeza uhusiano mzuri baina ya hospitali hiyo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia wizara hiyo.

Alisema kuwepo kwa madaktari hao, kumeongeza tija kubwa kwa jamii ya Wazanzibar wenye mahitaji ya huduma zao.

Mwinyi, alisema kuwasili kwa madaktari hao nchini ni fursa kwa wataalamu wa ndani kubadilishana uzoefu, kujengeana uwezo na kupunguza gharama kubwa kwa wagonjwa ya matibabu.

Mkurugenzi wa MIOT, Dk. Prithvi Manawng Mohandas, alizitaja huduma wanazotoa kwa wagonjwa wa visiwani hapa kwa saratani kuwa ni tiba za mionzi, kikemia, eneo maalum na matibabu ya moyo.

Akizungumzia kuhusu kiharusi, Dk. Prithvi, alisema wanatibu kwa kuwasaidia wagonjwa kuimarisha na kurejesha uwezo wa viungo vyao kwa kutembea na kufanya shughuli za kawaida kwa maisha yao ya kila siku.

# Kusini Unguja wahimizwa kutunza mazingira

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud amewataka wananchi kuhifadi na kutunza mazingira kwa manufaa ya jamii na Taifa.

Mahmoud alitoa rai hiyo wakati akikabidhi vifaa vya kilimo cha umwagiliaji kwa shehia nne za wilaya ya kati mkoani humo katika Kisiwa Cha Uzi.

Alisema vifaa hivyo vimetolewa na Jumuiya ya Misitu Pemba kwa ajili ya kuendeleza kilimo biashara ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa Zan adapt kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kazi ya uhifadhi wa misitu ni kubwa na inahitaji utumwa kwa sababu wanaohifadhi misitu hawapewi malipo ya fedha bali wanaonufaika ni wahifadhi wa Msitu wa Taifa wa Jozani.

Mohamoud, alisema wahifadhi hao wananufaika kwa kulipwa ada na watalii wanaotembelea msitu huo .

"Katika Mkoa wetu wa Kusini Unguja tuna wastani wa hifadhi za serikali nne, na tuna hifadhi kuu ya serikali moja, tunahifadhi za wananchi 32, hii ni kazi kubwa na tujipongeze sana Wanakusini Unguja kwa kweli tumejali mazingira yetu, maisha yetu na vizazi vijavyo," alisema Mahmoud.

Alisisitiza kuwa mazingira ni sehemu ya maisha ya wananchi, hivyo wanapaswa kuungwa mkono kwa utekelezaji wa mradi huo.

Alisema hatua ya shehia hizo nne kupatiwa miche ya miti ya matunda, ya asili, mimea na vifaa vya maji itachochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini hasa wa ukanda wa pwani.

Aliwataka wakazi wa shehia hizo kuthamini juhudi hizo za wadau wa maendeleo na kutumia vifaa hivyo kuleta tija na kutumika kwa muda mrefu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo Mkurugenzi wa jumuiya hiyo, Mbarouk Mussa Omar, alisema mradi huo unatekelezwa katika shehia hizo za Unguja na Pemba kukuza uchumi wa wanawake na vijiji vya ukanda wa pwani kupitia mbinu vumilivu ya mabadiliko ya tabia ya nchi.

Alisema alisema jumuiya hiyo inashirikiana na wadau wengine kutekeleza mradi huo, kikiwemo Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar) kuwasaidia wakulima wadogo hasa wanawake kupambana na umaskini na mabadiliko ya tabianchi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo, Ali Khamis Juma, alisema utekelezaji wa mradi huo unakwenda sambamba na sera ya serekali ya kuimarisha kilimo biashara na kunufaisha wananchi.

# Janabi: Tuwasubiri WHO watangaze

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, amesema wakati utakapofika wa kuwania kiti cha kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, ataweka wazi aliyonayo.

Prof. Janabi aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu huduma zinazotolewa na hospitali hiyo, pia mafanikio na changamoto katika mwaka 2024 na matarajio.

"Muda ukifika nitajibu kuhusu WHO. Nitajibu maswali vizuri, kwa sasa sitajibu vizuri, tusubiri WHO watangaze," alisema.

Hata hivyo, Prof. Janabi alisema hana wasiwasi na atakaowaachia kijiti, akisisitiza: "Nitakapomaliza muda au kukiwapo mabadiliko, nina imani hakuna kitakachoharibika kutokana na mfumo uliopo, mimi huwa ninasafiri hata wiki lakini niliowaacha wanafanya vizuri."

Rais Samia Suluhu Hassan, akiwaapisha mawaziri na viongozi wengine aliowateua hivi karibuni, alimtaja Prof. Janabi kujiandaa kuchukua kiti kilichoachwa wazi na Dk. Faustine Ndugulile, aliyefariki dunia Novemba 27 mwaka huu.

Dk. Ndugulile, aliyekuwa mtaalamu wa afya ya umma na Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, alishinda nafasi hiyo, akiwa mmoja wa wagombea watano waliojitokeza kumrithi Dk. Matshidiso Moeti, raia wa Botswana.

Prof. Janabi pia alisema pamoja na mafaniko yalikofikiwa, ikiwamo kupunguza rufani za huduma bobezi na za kibingwa nje ya nchi kwa takribani asilimia 90, changamoto zilizopo sasa ni uwezo mdogo wa wagonjwa kulipia huduma.

Alisema katika taaluma yake, amebaini sababu kuu ya magonjwa kwa wagonjwa walio wengi ni mtindo wa maisha, unaosababishwa na mlo duni, kutofanya mazoezi, hivyo kukumbwa na magonjwa yasiyoambukiza (NCD).

"Miaka 1990 nikasema ninakwenda kutibu watu, lakini nikaona kuna kitu kinakosekana, nikaenda kuwa mbobezi. Ila miaka tisa iliyopita alikuja mama mmoja, mwanawe ameganda, amepata degedege. Nilipomwona nikaona kweli alikuwa anachoka.

"Kuna kipimo cha kupima kiwango cha maji kwenye uti wa mgongo. Huyu mtoto tulibaini alikuwa na upungufu wa madini chuma na alikuwa na upungufu wa vitamini D ambayo husababishwa na calcium kushuka chini.

"Kasoro ni nini? Ni katika ulaji wa mtoto, nikamwambia Dk. Juma, sioni hii iko sawa, kuna kitu tunakosa. Nikamwambia kuna umuhimu wa kuwa na elimu kuhusu lishe.



"Mtoto wa rafiki yangu angekufa kwa ajili ya vitamin D tu! Kitu kidogo na degedege inaweza kusababishwa na vitu vingi. Mtindo wa maisha unaweza kukuondolea tatizo ulilokuwa nalo.

"Pili, miaka miwili iliyopita nilikwenda Hijja Mecca, kwenye ndege kuelekea huko nilikutana na Mbunge wa Jimbo la Mbagala, Abdallah Chaurembo, akaniambia 'nina kisukari aina ya pili'.

"Aina ya kwanza unazaliwa nayo na aina ya pili kuna sababu nyingi ukishakuwa mkubwa, niwaeleze 'hemoglobin A1C (HbA1c)' ni kipimo hiki kinatoa takwimu ya kisukari chako kuanzia Septemba hadi sasa (Desemba). Ikiwa saba kuna dalili za ugonjwa, tujenge taratibu kuangalia afya," alisema Prof. Janabi na kuongeza:

"Nikamwambia (mbunge) mimi naweza kukifanya kisukari chako kipotee. Tunakokwenda tutakaa wiki tatu, uwe na mimi mwanzo wa Hijja hadi mwisho tukiwa Mecca. Sasa yuko sawa, amerekebisha mtindo wa maisha."

Prof. Janabi pia alionya umma kuhusu ulaji wa vyakula vyenye protini zaidi itokanayo na wanyama, hasa msimu huu wa sikuu za mwisho wa mwaka ambao wengi hutumia muda mwingi kula mlo zaidi, akisema duniani kuna vifo milioni 34.6 miongoni mwao saratani milioni 9.5; magonjwa ya moyo milioni 17.9; presha milioni 7.5; kiharusi milioni tano na kisukari milioni 4.2.

"Tunasafisha figo MNH kila siku kati ya watu 120 hadi 150 kwa siku. Asilimia zaidi ya 90 ya hao wagonjwa ni presha, kisukari, unywaji holela dawa, magonjwa ya kuambukiza. Dola bilioni 1.4 ni fedha ambazo Afrika hutumia kwa mwaka kuwapeleka nje watu wake kutibiwa," alionya.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MEHRAN SHIRAZI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 458 ARY** aina ya **TOYOTA PREMIO.** Chassis namba **AT21000115713.** Engine namba **4A4875468.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi:

**PHQ/ARU/ARU/47597/2024.**



**TANGAZO LA MNADA**

**Marmbato,Mofano,Freemind,Jackeri,JJ,Blueflamingo na Kasaroba auctioneer Company** Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya Mnada Wa nyumba na magari Jijini Dar es saalam, Morogoro na Pwani Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 za hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| | Jina la mteja | Aina ya dhamana | Mahali ilipo | Dalali | Tarehe ya Mnada |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Agnes Robert Shawa | Toyota Klugger-T783DNW | Morogoro | Marmbato | 27.12.2024 |
| 2 | Yusuph Hemed Kamote | Toyota Fun cargo -T896DQR | Dar es salaam | Mofano | 27.12.2024 |
| 3 | Joha Haruna Thabiti | Nissan Navara-T396DTH | Dar es salaam | Freemind | 27.12.2024 |
| 4 | Diana Albert John | Nissan Navara-T334EAG | Dar es salaam | JACKERI | 27.12.2024 |
| 5 | Rukwaro Othniel Senkoro | Nissan Pathfinder-T143DCR | Dar es salaam | JJ | 27.12.2024 |
| 6 | Rashda Hasani Msigiti | Nyumba ipo Goba Luis | Dar es salaam | Blueflamingo | 27.12.2024 |
| 7 | Mwahila Cyprian Nyeshile | Nyumba ipo kibaha | Pwani | Kasaroba | 27.12.2024 |
| 8 | Mussa Abel Mange | Toyota coaster -T917DVY | Dar es salaam | DC classic | 27.12.2024 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya Tangazo.

**Kwa Mawasiliano Piga 0677014355 (Fanikiwa)**




Balozi wa Sweden nchini, Charlotta Ozaki Macias (katikati), akizungumza baada ya ubalozi huo, kutiliana saini makubaliano na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuendeleza haki za jinsia na uzazi. Kushoto ni Mwakilishi Mkazi wa UNFPA, Mark Bryan Schreiner na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya ubunifu na masuala ya afya ya Sahara Ventures, Jumanne Mtambalike. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kungwi afariki akienda kumfunda bibi harusi

**Na Oscar Assenga,** HANDENI

WATU wawili wamefariki dunia kwa ajali akiwamo kungwi, Mwanahamisi Mbelwa (40) aliyekuwa akienda kumfunda bibi harusi.

Ajali hiyo iliyotokea juzi, ilihusisha bodaboda na lori la mafuta eneo la Kwediyamba, Halmashauri ya Mji wa Handeni mkoani Tanga.

Kwa mujibu wa mashuhuda, ajali hiyo ilitokea wakati dereva wa bodaboda akijaribu kulipita lori, hivyo kushindwa baada ya kuteleza na kuingia uvunguni mwa gari hilo, hivyo kusababisha kufariki dunia.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Handeni, Dk. Stephen Julius, alisema walipokea miili ya watu wawili ambao walifariki dunia kabla ya kufikishwa hospitalini.

Ilielezwa kuwa Mwanahamisi ambaye ni kungwi, alikuwa akienda kwenye harusi wilayani humo kabla ya kukutwa na mauti.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Mchunguzi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na vifo hivyo.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa bodaboda kutaka kulipita lori lililokuwa mbele yake na kuteleza.

Kamanda Mchunguzi alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi zaidi wa tukio hilo huku akiwataka madereva kuzingatia na kutii sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali.

# RC alia vijana 30,000 hawataki kufanya kazi

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

MKOA wa Tanga unakabiliwa na changamoto ya vijana wapatao 30,000 ambao hawataki kutafuta kazi na kusoma na kuwa mzigo katika familia zao na taifa.

Changamoto hii ni moja ya mambo yaliyomo katika hotuba ya Mkuu wa Mkoa huo, Balozi Batilida Buriani iliyosomwa wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Vijana Wilaya ya Tanga uliofanyika jana katika viwanya vya Shule ya Kimataifa ya Tanga.

Balozi Batilda alisema kuwa katika Jiji la Tanga, tatizo la ajira kwa vijana ni changamoto inayolikabili, hivyo hawana budi kupambana nayo kwa nguvu zote kwa kushirikisha serikali na wadau wengine wa maendeleo.

Alisema kuwa kulingana na sensa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), changamoto ya ajira kwa vijana ni kubwa na kila mmoja anahitajika kuchukua hatua, wakiwamo vijana wenyewe kutafuta ajira na kujiajiri.

Alisema takwimu hizo za NBS zinaonesha kuwa kati ya vijana 147,000 wenye umri wa miaka 15-35 katika jiji hilo, ni 109,000 walioajiriwa katika sekta rasmi na isiyo rasmi.

"Lakini wapo takriban 5,000 wanatafuta kazi kwa sasa. Inasikitisha sana kuona kuwa kuna vijana takriban 30,000 hawatafuti kazi na wala hawataki kusoma. Hili ni tatizo la kijamii na ni lazima tushirikiane kulitatua," alisema.

## HABARI KIMATAIFA

# Pesa za kigeni zatoweka Syria

**DAMASCUS,** Syria

WAZIRI Mkuu wa Serikali ya mpito Syria, Mohammed al-Bashir, amekiri kwamba nchi haina pesa za kigeni na kusababisha kuwa vigumu kuwapa huduma za msingi raia wake.

Hata hivyo, Al-Bashir amewatolea wito raia wote wa nchi hiyo waliokimbilia mataifa mbali mbali kurejea nyumbani, baada ya kuangushwa utawala wa Bashar al-Assad.

Akizungumzia ukosefu akiba ya pesa ya kigeni, kiongozi huyo alisema licha ya kuwa na tatizo hilo, bado lengo lake la kutaka kuwalinda raia wote wa Syria na kuwapa huduma za msingi bado litabaki palepale.

**Tutawafuata Syria, na tunaomba nchi ziwakabidhi waliokimbia ili tupate haki.**

Hata hivyo, jumuiya ya kimataifa bado inafuatilia kwa karibu hali inayojitokeza nchini humo, huku Mawaziri wa Umoja wa Mambo ya Nje wa Umoja wa Ulaya wanapanga kuujadili mgogoro huo leo nchini Ujerumani.

Wakati huo huo Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken, amefanya ziara Jordan na Uturuki kwa ajili ya kuzungumzia mgogoro huo.

Qatar ilisema itafungua tena hivi karibuni ubalozi wake mjini Damascus.

Katika hatua nyingine, vikosi vya waasi wa Syria vilisema vinapanga kufunga magereza zinazojulikana kwa ukatili zilizoendeshwa na rais aliyeondolewa madarakani Bashar al-Assad na kuwasaka waliohusika katika mauaji au mateso kwa wafungwa.

Kiongozi wa vikosi vya waasi, Ahmed al-Sharaa, anayejulikana pia kama Abu Mohammed al-Jolani, pia alisema atavifuta vikosi vya usalama vya utawala wa zamani.

Video zinazoonyesha maelfu ya wafungwa wakiachiliwa huru kutoka gereza la Saydnaya, linalojulikana kama kichinjio cha binadamu na makundi ya kutetea haki za binadamu.

Takriban watu 60,000 waliteswa na kuuawa katika magereza yanayosimamiwa na Assad, shirika la kutetea haki za binadamu la Syria lenye makao yake nchini Uingereza lilisema.

Kundi la wapiganaji wa Kiislamu la Jolani, Hayat Tahrir al-Sham (HTS), liliongoza makundi mengine ya waasi wa Syria katika mashambulizi ambayo yalipindua utawala wa miaka 54 wa ukoo wa Assad.

Assad alikimbilia Russia Jumapili, akiwa na familia yake na kupewa hifadhi, baada ya waasi kuuteka mji mkuu Damascus. Katika taarifa yake tofauti, Jolani alisema msamaha kwa walioshiriki kuwatesa au kuwaua wafungwa hauingii akilini.

"Tutawafuata Syria, na tunaomba nchi ziwakabidhi waliokimbia ili tupate haki," alisema. **DW**

## Russia kutumia tena kombora jipya

**KYIV,** Ukraine

WASIWASI umewakumba raia wa Ukraine kushambuliwa na mapombora mapya kutoka Russia, baada ya nchi hiyo kutumia silaha za milipuko zilizotengenezwa nchini Marekani.

Russia inaweza kutumia tena makombora ya Oreshnik, kuishambulia Ukraine katika siku zijazo, katika kulipiza kisasi baada ya jeshi la nchi hiyo kutangaza kutumika makombora ATACMS dhidi ya ardhi yake.

Shirika la habari la Associated Press na Reuters liliripoti kuwa Wizara ya Ulinzi ya Russia, iliahidi kujibu kutokana na shambulio la Jeshi la Ukraine la makombora ya ATACMS ya Marekani kwenye uwanja wa ndege ulioko Taganrog.

Juzi, mashirika ya kimataifa ya habari AP na Reuters, yakinukuu chanzo katika serikali ya Marekani, kikieleza Russia inaweza tena kutumia mfumo wa makombora ya Oreshnik dhidi ya Ukraine katika siku zijazo.

Wakati huo huo, chanzo cha Reuters kilisisitiza kuwa matumizi ya mfumo mpya wa makombora ya Russia hayatabadilisha hali katika mstari wa mbele wa mapigano.

Shirika la habari la Associated Press, lilieleza kuwa Ukraine ina mfumo huo wa makombora machache pekee", na vifyatuzi vyake vina nguvu ndogo ya uharibifu kuliko ile ambayo jeshi la Russia hutumia nchini Ukraine mara kwa mara.

Awali, Rais wa Urusi Vladimir Putin alisema kuwa idadi ya kutosha ya mifumo kama kombora la Oreshnik itapunguza haja ya kutumia silaha za nyuklia. **BBC**



Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, akiwa na Rais wa Somalia,Hassan Mohamud na Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, baada ya mkutano walioafikiana kuhusu mgogoro wa nchi zao. **PICHA: REUTERS**

## Rais Yoon bado atetea kutumia sheria kijeshi

**SEOUL,** Korea Kusini

RAIS wa Korea Kusini, ambaye amekumbwa na mgogoro wa uongozi, Yoon Suk Yeol, ametetea uamuzi wake wa kuamrisha sheria ya kijeshi kutumika katika nchi hiyo wiki iliyopita.

Katika hotuba yake aliyoitoa jana, Rais Yoon Suk, alisema hatua aliyoichukua ililenga kuilinda demokrasia ya nchi hiyo.

Hotuba hiyo ambayo haikutarajiwa, iliyotangazwa na televisheni ya taifa, kiongozi huyo alisema jaribio hilo lilikuwa ni uamuzi wa kisheria wa kuzuia kuporomoka kwa demokrasia na kukabiliana na udikteta wa bunge unaoongozwa na upinzani.

Hata hivyo, Rais Yoon Suk, alisisitiza hatajiuzulu licha ya kuwepo kwa shinikizo la kumtaka kufanya hivyo.

"Nitasimama kidete iwapo nitashtakiwa au kuchunguzwa. Nitapigana hadi mwisho" alisema.

Rais huyo na washirika wake kwa sasa wanakabiliwa na uchunguzi kuhusu mashtaka ya uasi, na walipigwa marufuku ya kusafiri.

Mashataka hayo yamepingwa vikali na Yoon akieleza kuwa amri yake ya sheria ya kijeshi haikuwa kitendo cha uasi, na kuwalaumu wapinzani wake wa kisiasa kutengeneza uchochezi na uwongo ili kuangusha serikali yake.

Katika hotuba yake, ambayo ni ya kwanza tangu alipoomba radhi Jumamosi iliyopita, alirudia hoja zilezile alizotumia alipotangaza sheria ya kijeshi, kwamba upinzani ni hatari na kwamba kwa kuchukua udhibiti, amekuwa akijaribu kuulinda umma na kutetea demokrasia. **BBC**

HABARI MICHEZO

# 'BASI' LA PAMBA LAMSHANGAZA KOCHA WA JKT TANZANIA FC

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, amesema mfumo wa 'kupaki basi' ndiyo iliyowaokoa Pamba Jiji FC wasifungwe juzi kwenye mchezo wa Ligi Kuu, huku akiwasifu kuwa walikuwa bora sana kwa mpango kazi huo.

Akizungumza mara baada ya timu yake kutoka suluhu nyumbani, Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo,Dar es Salaam, Ahmad alimsifu kocha Fred Minziro kwa kucheza muda mrefu akiwa nyuma ya mpira, hivyo kuvuruga mipango yote ambayo alikuwa ameipanga

**"Nawapongeza wapinzani wetu, walikuja hapa kwa lengo la kuisaka pointi moja kwa kukaa nyuma, wameipata, na sisi sasa tunajipanga kwa mchezo ujao," alisema kocha huyo.**

Hata hivyo alisema kwa nyakati kadhaa walipata nafasi za kufunga, lakini kwa bahati mbaya wachezaji wake hawakuwa watulivu, vinginevyo wangeweza kushinda mchezo huo.

"Tulikuwa vuzuri kwenye mchezo huu, utulivu wa wachezaji wangu ndiyo uliokosekana, kama wangetulia ilikuwa tushinde mechi hii bila matatizo yoyote," alisema kocha huyo.

Kwa upande wa Minziro, alikiri kucheza wakiwa nyuma ya mpira, mfumo ambao uliwasaidia tofauti kama wangeamua kupishana nao.

"Leo tumecheza vizuri, nimewaheshimu JKT Tanzania, wana timu nzuri, wamesajili wachezaji wazuri, lakini kila muda na dakika zilivyozidi kwenda mbele ndiyo tulivyokuwa wazuri zaidi dhidi ya wapinzani wetu," alisema.

Suluhu hiyo, imezifanya timu hizo kupanda nafasi moja juu kila moja.

JKT Tanzania iliyokuwa kwenye nafasi ya nane na pointi 16, imepanda hatua moja hadi nafasi ya saba ikiwa na pointi 17, ikicheza michezo 12, huku Pamba Jiji ambayo awali ilikuwa kwenye nafasi ya 13, imepanda hadi nafasi ya 12 ikiwa na pointi 12, ikicheza michezo 14 mpaka sasa.

Pamba imebakisha mchezo mmoja tu imalize mechi zake za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.

Mchezo wake huo wa mwisho, unatarajiwa kupigwa kwenye Uwanja wa KMC Complex dhidi ya wenyeji KMC.



Wachezaji wa Timu ya Kitunda FC, wakiwania mpira walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda jijini Dar es Salaam jana kujiandaa na michuano ya ligi Daraja la Tatu inayoendelea. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Coastal Union yaitisha Fountain Gate

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Coastal Union imesema hawana sababu ya kutopata ushindi kwenye mchezo wa leo wa Ligi Kuu dhidi yaFountain Gate utakaochezwa kwenye uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati.

Akizungumza na Nipashe jana, mara baada ya kuwasili mkoani Manyara, Msemaji wa timu hiyo, Abbas El Sabri alisema malengo yao ni kupata pointi tatu katika mchezo huo.

"Tunashukuru tumefika salama asubuhi hii kwa ajili ya mchezo wetu wa kesho (leo), malengo yetu ni kupata pointi tatu ugenini, hatuna sababu ya kutofanya hivyo," alisema El Sabri.

Aidha, alisema licha ya kutambua kuwa mchezo huo utakuwa mgumu, lakini benchi la ufundi na wachezaji wao wamejiandaa vizuri na kila mmoja ana morali ya juu.

"Kila mmoja kwenye kikosi anautaka huu mchezo, ni mchezo ambao tunaona tunastahili kupata alama tatu," alisema.

Aidha aliwaomba mashabiki wao waendelee kuwaunga mkono kwa kujitokeza kwa wingi uwanjani kwenye michezo yao ili kuwapa ushirikiano wachezaji wao.

"Tunaomba mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi uwanjani kwa lengo la kuwapa sapoti wachezaji wetu waweze kupata nguvu ya kupambania ushindi katika kila mchezo tukianza na huu dhidi ya Fountain Gate," alisema El Sabri.

Alisema Ligi Kuu msimu huu ina ushindani kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kila timu.

# Matumla atamba kumpiga Mlawa

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Amiri Matumla 'Nyoka Mtoto' ametamba kumpiga vikali mpinzani wake Anuary Mlawa kwenye pambano lao la 'Boxing Day' litakalofanyika Desemba 26 kwenye uwanja wa Zimbile mkoani Kagera.

Akizungumza na Nipashe jana, Matumla alisema amejiandaa kurudisha heshima ya kwao Keko sehemu aliyozaliwa na kukulia kwa kumpa kipigo cha aina yake mpinzani wake huyo.

Miaka ya nyuma Keko ilikuwa ikisifika kuzalisha mabondia wengi waliokuwa wakitamba hapa nchini kuanzia kizazi cha Rashid Matumla.

"Malengo yangu ni kuibuka na ushindi siku hiyo kwani nataka nirudishe heshima ya Keko kupitia pambano hilo," alisema Matumla.

Alisema kutokana na mazoezi anayoendelea kuyafanya anaamini atawapa burudani mashabiki wake na kuwataka wajitokeze kwa wingi siku hiyo.

Aliongeza kuwa hana wasi wasi na mpinzani wake kwa kuwa anamfahamu vizuri hivyo anajiamini na kile atakachokwenda kukifanya.

"Sina wasi wasi na mpinzani wangu ninamfahamu vyema kwani nimefuatilia mapambano yake na kugundua udhaifu wake ambao naweza nikautumia kumpiga, naomba mashabiki wangu waendelee kuniombea dua, alisema.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**LIVERPOOL YAMTAKA PEDRO**

LIVERPOOL imemefanya usajili wa mshambuliaji wa Brighton wa Brazil, Joao Pedro, 23, kuwa kipaumbele kwa msimu ujao. ***(Universo Online)***

**RASHFORD APANGIWA BEI**

KLABU ya Manchester United inataka pauni milioni 40 kwa ajili ya Marcus Rashford, 27, lakini wanajua kwamba hakuna uwezekano wa kupata mnunuzi yeyote wa mshambuliaji huyo Januari. ***(Mail)***

**DAVIES AOTA MBAWA MADRID**

REAL Madrid imepoteza matumaini ya kumsajili beki wa kushoto wa Bayern Munich kutoka Canada, Alphonso Davies, 24. ***(Goal)***

**AWANIWA CRYSTAL PALACE**

KLABU ya Crystal Palace ina nia ya kumnunua winga wa Fluminense na Colombia, Jhon Arias, 27, kuelekea dirisha la uhamisho la Januari. ***(Football Insider)***

**YAMTAKA VLAHOVIC**

KLABU ya Manchester United imemuongeza mchezaji wa kimataifa wa Serbia na Juventus, Dusan Vlahovic, 24, kwenye orodha yao ya washambuliaji wanaowataka. ***(Football Insider)***

**REINILDO AWINDWA ENGLAND**

KLABU nyingi za Ligi Kuu England zinamfuatilia beki wa kushoto wa Msumbiji, Reinildo, 30, ambaye mkataba wake na Atletico Madrid unamalizika msimu ujao. ***(Goal)***

**YAVUTIWA NA NUAMAH**

KLABU za Crystal Palace, Everton na Fulham zote zinavutiwa na winga wa Lyon, Ernest Nuamah, 21. ***(Foot Mercato)***

**KUONGEZEWA MKATABA**

WOLVES inataka kumuongezea mkataba beki wake wa kulia raia wa Ureno, Nelson Semedo, 31. ***(Express & Star)***

**CASADEI KWA MKOPO JUVE**

KLABU ya Juventus inafikiria kumsajili kiungo wa Chelsea, Cesare Casadei, 21, kwa mkopo. Muitaliano huyo pia amekuwa akihusishwa na klabu ya Serie A ya Monza. ***(Calciomercato)***

**MAN U HAWANA HARAKA**

MANCHESTER United haina haraka ya kuleta mbadala wa Dan Ashworth kama mkurugenzi wa michezo na wanaamini kuwa wana watendaji wenye uwezo ambao wanaweza kuchukua majukumu yake. ***(Teamtalks)***

**WEST HAM KUSAJILI MBADALA**

KLABU ya West Ham inafikiria kumsajili mshambuliaji kwa mkopo Januari kufuatia mchezaji wa kimataifa wa Jamaica, Michail Antonio, 34, kuuumia katika ajali. ***(Give MeSport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HAKUNA UHAKIKA DE JONG KUBAKI BARCA

**Kocha wa Barcelona Hansi ameweka wazi kuwa hana...**

**BARCELONA,** Hispania

HANSI Flick amesema anamthamini Frenkie de Jong kama mchezaji wa kikosi cha Barcelona lakini ameweka wazi kuwa hawezi "kudhibiti kinachotoka nje" huku Mholanzi huyo akiendelea kuhusishwa kutaka kuondoka Katalunya.

**Kiungo huyo wa zamani wa Ajax aliwasili Camp Nou mwaka 2019 baada ya kuonesha kiwango kizuri wakati wa timu yake ya zamani ilipofika hadi nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.**

Ameshinda taji moja la LaLiga pamoja na Copa del Rey na ushindi wa Supercopa de Espana, lakini mara nyingi amekuwa akihusishwa na kuondoka.

De Jong alikuwa akitajwa kuwania na klabu ya Manchester United siku za nyuma, huku vyombo vya habari vikiangazia hali ngumu ya mkataba wake huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akionyesha mara kwa mara kutaka kubaki.

Na sasa kocha huyo wa zamani wa Bayern Munich amesema: "Kwangu mimi yeye De Jong ni mchezaji muhimu sana. Hayo ni maoni yangu na siwezi kudhibiti kile kinachotoka nje."

Hivi majuzi ilidaiwa kuwa Barca wanataka kumtoa De Jong msimu ujao wa joto kutokana na mkwamo wa mkataba mpya, huku ripoti pia zikipendekeza wababe hao wa Katalunya wanaweza kukubali ada ya uhamisho ya chini ya pauni milioni 20 ili kumtoa kwenye vitabu vyao.

Jeraha kubwa alilolipata Aprili msimu uliopita lilimfanya mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi kukosa Euro 2024 na alirejea tu kwenye kikosi cha kwanza Oktoba, akianza michezo miwili pekee katika LaLiga na Ligi ya Mabingwa.



# GUARDIOLA HAELEWI KITU

**TURIN,** Italia

PEP Guardiola amesema anajiuliza maswali mengi kama kocha wa Manchester City baada ya timu yake kushuhudia ikichezea kichapo katika mechi saba kati ya 10 huku mabao ya Dusan Vlahovic na Weston McKennie yakiipa Juventus ushindi wa 2-0 kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya mjini Turin juzi.

City watasafiri hadi Paris Saint-Germain mwezi ujao wakijua kwamba kushindwa kunaweza kuwapeleka katika timu nane za mwisho kwenye msimamo wa Ligi ya Mabingwa na kuwaacha katika fedheha ya kutolewa katika michuano hiyo kabla ya awamu ya mtoano.

Dhidi ya timu ya Juventus ambayo ilikuwa imeshinda mchezo mmoja tu kati ya sita za awali katika mashindano yote, City ilijitahidi kutengeneza nafasi za kushinda, na majirani zao Manchester United wakiwafuata Etihad kwenye Ligi Kuu Jumapili, Guardiola alisema anaanza kujiuliza kwa kushindwa kwao.

"Bila shaka ninajiuliza. Nina mawazo yangu," alisema Guardiola. "Niko thabiti katika wakati mzuri na wakati mbaya. Ninajaribu kutafuta njia ya kufanya hivyo. Mimi ni mwaminifu sana. Ikiwa tunacheza vizuri, tunacheza vizuri.

"Chumba cha kubadilishia nguo kipo imara. Shinda tunafurahi, tushindwe hatuna. Tufanye nini, tujionee huruma. Hapana, tutajiboresha na kwenda mbele."

Licha ya kudorora kwa kiwango chake, ambacho ndicho kibaya zaidi katika maisha yake ya ukocha, Guardiola alisema kuwa hakuwa akikabiliwa na changamoto kubwa.

# Saudi Arabia kuandaa kombe la Dunia 2034




**NYON,** Uswisi

KOMBE la Dunia la 2034 litafanyika nchini Saudi Arabia na Kombe la Dunia la 2030 litafanyika kwa ushirikiano wa nchi tatu Morocco, Ureno na Hispania huku mechi tatu zitafanyika katika nchi tatu za Amerika Kusini, Shirikisho la soka la Kimataifa, FIFA, limethibitisha katika mkutano wake wa Jumatano.

Uamuzi huo ulitangazwa na rais wa FIFA, Gianni Infantino.

Fainali za Kombe la Dunia za 2030 na 2034 zilikuwa na ofa moja tu na zote mbili zilithibitishwa kwa shangwe na mashirikisho zaidi ya 200 ya FIFA.

"Tunaleta soka katika nchi nyingi na idadi ya timu haijapunguza ubora. Kwa hakika imeongeza fursa," alisema Infantino kuhusu Kombe la Dunia la 2030.

"Kura ya mkutano ni kubwa na ya wazi," alisema Infantino.

Saudi Arabia ilikuwa mzabuni pekee wa kombe la 2034 la mashindano hayo ya dunia.

"Huu ni wakati wa kihistoria kwa Saudi Arabia na ndoto imetimia kwa watu wetu wote milioni 32 ambao wanapenda mchezo huu," alisema Prince Abdulaziz bin Turki bin Faisal Al Saud, rais wa Kamati ya Olimpiki na Paralimpiki ya Saudia.

"Ufalme uko katika safari ya ajabu ya mabadiliko chini ya dira ya 2030 na leo (juzi) ni hatua nyingine kubwa mbele ambayo inaakisi na kusherehekea maendeleo yetu huku tukitazamia siku zijazo nzuri zaidi."

Mashirikisho wanachama 211 pia yalipewa chaguo pekee la kupiga kura kwa ajili ya kombe la dunia la 2030 ambapo Uruguay, Paraguay na Argentina nchi ambazo hapo awali zilitangaza zabuni ya kuandaa kila moja itakuwa mwenyeji wa mechi moja ili kuanza mashindano hayo.

Hii itaruhusu FIFA kuandaa mchezo wa ufunguzi katika mji mkuu wa Uruguay wa Montevideo, ambapo Uwanja wa Centenario uliandaa fainali ya kwanza ya Kombe la Dunia la 1930.

# Arteta kuingia sokoni Januari

**LIVERPOOL,** England

ARSENAL inaweza kutafuta wachezaji wapya wakati wa dirisha la Januari baada ya kuanza msimu wa 2024/25 wakiwa na majeruhi wengi.

Washikabunduki hao walianza msimu mpya wakiwa na matumaini makubwa baada ya kukaribia kubeba kombe la Ligi Kuu England msimu uliopita.

Hata hivyo, baada ya mechi 15, wanajikuta katika nafasi ya tatu nyuma ya Liverpool na Chelsea.

Majeraha yameathiri kikosi cha Mikel Arteta huku nahodha Martin Odegaard akiwa nje ya uwanja kwa takriban miezi miwili kutokana na jeraha la kifundo cha mguu na Ben White akiwa amefanyiwa upasuaji.

Riccardo Calafiori, Takehiro Tomiyasu, Gabriel na Oleksandr Zinchenko wote pia wamekosa michezo kutokana na majeraha msimu huu.


Lakini, kwa bahati nzuri kwa Arteta, dirisha la usajili la Januari sasa limebakiza wiki chache tu na linaweza kutoa fursa ya kusajili wachezaji wapya pale Emirates.

"Dirisha linatupa fursa ya kuimarisha timu ikiwa tunahisi hiyo inahitajika na tunahisi kuwa tuna uwezo wa kufanya hivyo pia," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Tupo kwenye hilo na inabidi tu kutathmini hali kwa sababu inabadilika kila wiki. Nina matumaini kwamba katika wiki chache tutakuwa katika mahali pazuri zaidi," alisema Arteta.

Dirisha la majira ya baridi la Arsenal limekuwa gumu kutokana na kuondoka ghafla kwa Mkurugenzi wa michezo Edu.

Hata hivyo, Jason Ayto ataongoza uajiri kabla ya mtaalamu mpya wa uhamisho kuteuliwa, huku Mkurugenzi wa zamani wa Manchester United, Dan Ashworth akiripotiwa kuwindwa na Washikabunduki hao.



HABARI MICHEZO

# TANZANIA WAVULANA U-15 MABINGWA CECAFA 2024

**Na Mwandishi Wetu,** KAMPALA

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wavulana ya umri chini ya miaka 15 imetwaa ubingwa wa mashindano ya Shule ya Afrika kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CAF CECAFA U-15) baada ya kuifunga Rwanda mabao 2-0 katika mechi iliyofanyika kwenye Uwanja wa St. Mary's Kitende jijini hapa jana.

Yosso hao wa Tanzania wametwaa ubingwa huo baada ya kufikisha pointi saba na kukata tiketi ya kushiriki fainali za Afrika (CAF U-15), zitakazochezwa mwakani.

Kwa ushindi huo Tanzania imepata zawadi ya Dola za Marekani 100,000 wakati nafasi ya pili katika michuano hiyo imeenda kwa wenyeji Uganda ambao wamepata Dola za Marekani 75,000.

**Nafasi ya tatu kwa wanaume imechukuliwa na Somalia na kujipatia zawadi ya Dola za Marekani 50,000.**

Kwa upande wa wasichana wenyeji Uganda wameibuka mabingwa baada ya kuitwanga bila huruma Rwanda mabao 8-0 na kufikisha pointi saba sawa na Tanzania iliyomaliza katika nafasi ya pili kufuatia ushindi wa gold 1-0 dhidi ya Burundi.

Timu hiyo ya wasichana ya Uganda ilipata zawadi ya Dola za Marekani 100,000 huku Tanzania wakiondoka na Dola za Marekani 75,000.

Nafasi ya tatu kwa upande wa wasichana ilichukuliwa na Burundi iliyomaliza ikiwa na pointi tatu na kujinyakulia zawadi ya Dola za Marekani 50,000.

Rwanda wavulana walipata tuzo ya 'Fair Play' wakati kwa wasichana ilienda kwa Burundi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa CECAFA, Duka Gecheo, amesema mashindano haya yamefanyika katika kiwango cha juu na timu zote zilizoshiriki zimeonyesha kiwango bora.

Gecheo anasema michuano imezidi kuwa bora ikilinganishwa na mwaka uliopita.

"Tunafuraha kumaliza mashindano vyema, haya ni mafanikio makubwa sana kwetu, hii inatupa nafasi ya kuwa na michuano ya U-17 bora zaidi, wachezaji wanakuwa wamepata uzoefu.

Aliongeza anaamini mashindano ya U-17 yanayotarajiwa kuanza kesho jijini hapa yatakuwa na ushindani pia.



Mtoto akifanya mazoezi ya kucheza 'tenis' katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam kama alivyokutwa na mpiga picha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TOC yatoa maagizo vyama vya michezo

**Na Renatha Msungu** DODOMA

KAMATI ya Olimpiki Tanzania (TOC) imeviagiza vyama vya michezo na mashirikisho hapa nchini, kuandaa mashindano ya michezo yaliyopo ndani ya kalenda zao za mwaka ili kupata nafasi ya ushiriki wa michuano ya kimataifa inayoandaliwa na mashirikisho ya michezo duniani.

Hayo yalisemwa na Katibu wa TOC, Filbert Bayi, wakati wa ufunguzi wa semina elekezi ya makatibu wakuu wa vyama vya michezo na mashirikisho hapa nchini uliofanyika jana mkoani hapa ukiwa na lengo la kuvikumbusha vyama kutekeleza wajibu wao kwenye michezo.

Bayi alisema, vyama hivyo vinapaswa kuwa hai kwa kulipa ada, kuandaa mashindano ambayo yapo kwenye kalenda zao pamoja na kushiriki mashindano ya kirafiki yanayoandaliwa kimataifa ili waweze kutambulika na mashirikisho ya kimataifa.

"Vyama mnapaswa kulipa ada ili muweze kuwa hai na kutambulika na mashirikisho yenu, igeni mfano wa vyama ambavyo vinatimiza wajibu wao na kupata mialiko ya ushiriki wa michuano ya kimataifa,"alisema Bayi.

Bayi alivitaja baadhi ya vyama ambavyo vinafanya vizuri ni pamoja na Shirikisho la Riadha nchini (RT), Shirikisho la mpira wa kikapu(TBF), Shirikisho la Soka nchini (TFF) pamoja na vyama vingine ambavyo vimekuwa vikitekeleza masharti yaliyopo ndani ya mchezo husika.

Aidha alisema baada ya semina hiyo elekezi vyama ambavyo havishiriki wala kuandaa mashindano yoyote ya ndani vinapaswa kuanza kuandaa ili kuhakikisha msimu wa michuano ya kimataifa unapowadia na wao washiriki.

Kwa upande wake, Rais wa TOC, Gulam Rashid alivitaka vyama hivyo katika chaguzi zao wanazofanya kuzingatia jenda ili kupata viongozi wanawake na wanaume ambao wataongoza yama hivyo kwa kadri katiba yao inavyowaeleleza.

Gulam alisema vyama vingi vimekuwa na uongozi usiozingatia jenda hivyo katika chaguzi zijazo za vyama hivyo vya michezo wanapaswa kuliangalia hilo ili kupata viongozi wanawake ambao watafanya ushawishi wa kuibua wachezaji chipukizi wanawake.

"Nawapongeza kwa kuhudhuria semina hii elekezi kwa vyama vya michezo, lakini nawashauri mzingatie jenda katika vyama vyenu pale mnapofanya uchaguzi wa viongozi,"alisema Rashid.

Kwa upande wake katibu wa Shirikisho la riadha Zanzibar, Muhidin Yasin Masunzu aliishukuru TOC kwa kuandaa semina hiyo elekezi kwa makatibu wakuu wa vyama vya michezona mashirikisho ambapo alisema imesaidia kuvikumbusha vyama wajibu wao katika michezo.

## Fadlu aita mashabiki

INATOKA UK. 24

nafasi kubwa sana kwenye safari yetu ya kusonga mbele, litakuwa jambo lenye msisimko kuona uwanja umejaa, italeta hamasa kubwa kwa wachezaji kuweza kupambana katika dakika zote," alisema Fadlu.

Aidha, alisema matokeo ya mchezo wao uliopita dhidi ya CS Costantine ambao walipoteza kwa mabao 2-1 yamepita na sasa wanaangalia mchezo unaofuata ambao ni muhimu.

"Mchezo muhimu kwa sasa ni huu ambao upo mbele yetu, tunahitaji ushindi na si kingine, ukiangalia kundi letu linaonekana kuwa gumu sana," alisema Fadlu.

Alisema kwa namna msimamo wa kundi ulivyo mpaka sasa, kila timu ina nafasi yakusonga mbele kutegemea na matokeo watakayoyapata kwenye michezo iliyobakia.

CS Costantine inaongoza kundi hilo kwa kuwa na pointi sita, Simba na Bravos do Marquiz kila mmoja ana pointi tatu na anayeburuza mkia ni CS Sfaxien ambao hawana pointi huku kila timu ikiwa imecheza michezo miwili.

Wakati huo huo, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema wanaendelea na hamasa kwa mashabiki wao ili kuujaza uwanja siku ya mchezo.

"Huu ni mchezo muhimu sana, tunataka kuona mashabiki wanajaa sana uwanjani kuwapelekea moto waarabu, tumepania kupata pointi tatu ambazo ni muhimu sana kwetu, kila mwanasimba hakuna haja ya kubaki nyumbani jumapili, kila mmoja afike uwanjani kuwapa hamasa wachezaji wetu," alisema Ahmed.

## Yanga yaifuata Mazembe

INATOKA UK. 24

toa suluhu dhidi ya MC Alger ya Algeria, nyumbani, huku Yanga ikipoteza michezo yote miwili ya mwanzo kwa mabao 2-0 dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan na 2-0 dhidi ya MC Alger.

"Kikosi kiko sawa, majeruhi pekee ni Shadrack Boka, waliobaki ni wazima, kazi imebaki kwa kocha Sead Ramovic mwenyewe kuona nani atafaa na yupi anaweza kumtumia kwenye mchezo huo," alisema Kamwe.

Yanga inahitaji ushindi ili kuweka hai matumaini yao ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

# Michezo

Ijumaa Desemba 13, 2024

Nipashe




## Hakuna uhakika De Jong kubaki

UKURASA 21




Kikosi cha timu ya taifa ya Tanzania ya vijana chini ya miaka 15 wakiwa na kombe la ubingwa la michuano ya CAF kwa vijana ukanda wa CECAFA walioutwaa jana nchini Uganda baada ya kuifunga Rwanda mabao 2-0. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Yanga yaifuata Mazembe wakiwa na matumaini tele

## Waahidi kutoa jasho na kupambana kwa ajili ya pointi tatu huku...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga iliondoka nchini jana asubuhi kwenda Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kucheza mechi ya mzunguko wa tatu wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi ya TP Mazembe huku Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, akisema kitu pekee kitakachoisaidia timu hiyo kushinda ni kwa wachezaji wake kukubali kuvuja 'jasho na damu' dakika zote 90 za mchezo huo.

**Yanga kesho itakuwa mgeni wa TP Mazembe kwenye mchezo utakaoanza saa 10:00 jioni.**

Akizungumza kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Kamwe (pichani) alisema hakuna historia wala vijisababu vinavyoweza kuwasaidia kwa sasa zaidi ya wachezaji wao kujituma na kupata ushindi.

"Hatuondoki na rekodi ya mchezo wowote, hapa tulipofika hakuna rekodi yoyote inayoweza kutusaidia, kitakachotusaidia ni kuvuja kwa jasho letu kwenye mchezo huo, hakuna muda kutafuta vijisababu vya pembeni, ni muda wa kwenda kutokwa machozi, jasho na damu ili tupate matokeo mazuri.



Ni mechi ngumu, lakini hakuna namna ni lazima tuikabili, tuna imani tunaweza kupata matokeo mazuri dhidi yao, malengo yapo pale pale, kufuzu kwenye hili kundi, haijaisha na wala hatujachoka," alisema Kamwe.

Misimu miwili iliyopita timu hizo zilikutana mara mbili kwenye hatua ya makundi, Kombe la Shirikisho Afrika na Yanga kushinda michezo yote miwili, ikiichapa TP Mazembe mabao 3-1 Februari 19, mwaka jana Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na marudiano kushinda 1-0 kwenye uwanja wa ugenini.

Mchezo huo wa kesho utazikutanisha timu ambazo hazijapata ushindi wowote kwenye michezo iliyopita katika kundi lao.

Hata hivyo, TP Mazembe ina pointi moja iliyoipata kwa ku

INAENDELEA UKURASA 23

# Fadlu aita mashabiki kwa Mkapa

**Na Faustine Feliciane**

IKIWA imebaki siku moja kabla ya mchezo wao dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia, kocha wa Simba, Fadlu Davids amewataka mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi uwanjani kuwapa hamasa wachezaji wake katika mchezo huo muhimu.



Fadlu, alisema mchezo huo wa Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa Jumapili ni muhimu zaidi kwao kupata ushindi ili kuendelea kuweka hai matumaini ya mipango yao ya kucheza robo fainali ya michuano hiyo.

"Shabiki ana

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >